

CHAKITA 2013
KONGAMANO LA KIMATAIFA LA KISWAHILI
MAKARIBISHO

Tangu taifa la Kenya lipate uhuru mnamo Disemba 12, 1963 kumekuwa na hatua nyingi zilizopigwa ili kuimarisha Kiswahili kama lugha ya utambulisho wa utaiifa na kujenga hisia za uzalendo. Baadhi ya hatua hizo zinaonekana katika mfumo wa elimu ambapo Kiswahili hufundishwa na kutanihiwa shuleni na vyuoni. Kiswahili pia hutumiwa bungeni na katika biashara mbalimbali. Umilisi wa lugha hii miongoni mwa umma unatia moyo. Watu wengi wa makamo huongea Kiswahili kwa ufasaha kuliko ilivyokuwa siku za nyuma na mielekeo hasi kuhusu lugha yetu ya taifa inaendelea kupungua. Jambo la kutia moyo zaidi ni kwamba hivi majuzi, Katiba ya Kenya katika Ibara ya Saba imeipa lugha hii hadhi kubwa kama lugha ya taifa na rasmi. Hadhi hii inatoa fursa kwa umma kupata hudumu kupitia lugha ya taifa. Lakini inabidi sasa pawekwe mikakati madhubuti ya kutekeleza agizo hili la kikatiba. Watetezi wa Kiswahili, kwa ushirika na Wizara ya Michezo, Utamaduni na Sanaa, wako mbioni kuhamasisha umma kuhusu umuhimu wa Sera ya Lugha za Kenya. Uti wa mgongo wa sera hiyo ni fursa iliyopewa Kiswahili. Tunatumaini kwamba Wizara itakamilisha Sera ya Lugha na kuhimiza bunge ipitishie Sheria ya utekelezaji wa sera hiyo. Tungetaka kuona lugha ya Kiswahili ikitumika serikalini, bungeni, mahakamani na katika shughuli za kijamii. Hii ndiyo lugha inayoweza kujenga uwiano na utangamano wa kitaifa.

Ni kutokana na hisia hizi ambapo Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki, ikishirikiana na Chama cha Kiswahili cha Taifa (Kenya) wana furaha kuwakaribisha katika Kongamano hili la kuadhimisha miaka 50 ya Kiswahili Nchini Kenya. Katika Kongamano hili, tunatarajia kufikia maamuzi yatakayoonyesha namna tunavyoweza kuimarisha Kiswahili nchini Kenya na katika ukanda wa Afrika Mashariki. Penye nia pana njia. Tuna nia ya kuifanya lugha ya Kiswahili nyenzo ya maendeleo katika ukanda huu. Tunawashukuru wale wote waliotoa mchango ili kufanikisha kongamano hili.

Karibuni!

Prof. Kimani Njogu, Ph.D.

Mwenyekiti

Chama cha Kiswahili cha Taifa (CHAKITA) – Kenya

KAMATI ANDALIZI

Prof. Kimani Njogu, *Mwenyekiti*
Prof. Chacha Nyaigotti, *Mwanakamati*
Prof. Clara Momanyi, *Katibu*
Dkt. Chacha Mwita, *Mwanakamati*
Bi. Rose Mavisi, *Mwanakamati*
Bi. Lina Akaka, *Mwanakamati*

UONGOZI WA CHAKITA

Prof. Kimani Njogu, *Mwenyekiti*
Dkt. Mwanakombo Noordin, *Naibu Mwenyekiti*
Prof. Clara Momanyi, *Katibu*
Dkt. Issa Mwamzandi, *Naibu Katibu*
Prof. Naomi Shitemi, *Mweka Hazina*
Dkt. Mwenda Mukuthuria, *Naibu Mweka Hazina*
Dkt. Sangai Mohochi, *Mhariri mkuu*
Bw. S.K. Karani, *Naibu Mhariri Mkuu*
Prof. Inyani Simala, *Afisa Mwenezi*
Bi. Sheila Wandera-Simwa, *Naibu Afisa Mwenezi*

Wanakamati:

- Bw. Ali Njama
- Dkt. Njoroge Ngugi
- Bw. Bitugi Matundura
- Prof. John Habwe
- Dkt. Florence Indede

UFADHILI

Kamati Andalizi pamoja na Uongozi wa CHAKITA wangependa kutoa shukrani za dhati kwa mashirika yafuatayo ambayo yalichangia katika kufaulisha kongamano la mwaka huu:

- Longhorn Publishers
- Goethe Institut
- Catholic University of Eastern Africa (CUEA)
- Nation Media Group
- Oxford University Press
- Twaweza Communications
- Jomo Kenyatta Foundation

RATIBA YA KONGAMANO
JUMATANO, TAREHE 21 AGOSTI

2.00 – 2.45 Usajili

2.45 – 3.15 Kichocheo cha Kongamano

Mwenyekiti: Dkt. Leonard Chacha

Mada: Uchapishaji wa Vitabu vya Kiswahili

Wawezeshaji: James Mwilaria (Longhorn), Hassan Said (OUP), Kakai Karani (Bookmark)

3.15 – 4.15 *Ufunguzi: Mwenyekiti: Prof. Clara Momanyi - Mwenyekiti, Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki*

Hotuba Fupi: Prof. Kimani Njogu - Mwenyekiti, CHAKITA

Hotuba ya Makaribisho: Rev. Dkt. Pius Rutechura - Makamu Mkuu wa Chuo, Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki

Ufunguzi Rasmi: Dkt. Hassan Wario - Waziri wa Michezo, Utamaduni na Sanaa

4.10 – 5.00 *Hotuba Maalum: Prof. Abdulaziz Mohammed - Chuo Kikuu cha Nairobi*

Mada: Miaka Hamsini ya Kiswahili Kenya! Tumejifunza nini?

5.00 – 5.30 **CHAI**

5.30 – 7.00 **Shughuli za Majopo**

Jopo I (Ukumbi Mkuu): Vyombo vya Habari na Maendeleo

Mwenyekiti: Rose Mavisi

Mchango wa Redio na Runinga katika Makosa Yanayofanywa na Wanafunzi katika Uandishi wa Insha - *Daniel Kiprugut Ng'etich, Chuo Kikuu cha Kenyatta*

Mchango wa Vyombo vya Habari katika Maendeleo ya Kiswahili - *Ngugi Kariuki na Ontieri Omari, Chuo Kikuu cha Masai Mara*

Changamoto za Tafsiri katika Simu za Rununu - *John Marani, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro*

Matumizi ya Tarakilishi katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili Nchini Kenya - *Florence A. Miima, Rose Mavisi na Vincent F. Kawoya, Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki*

MJADALA

Jopo II (Chumba 01): Kiswahili Utamaduni na Maendeleo

Mwenyekiti: Dkt. Richard Wafula

Nafasi ya Mwaka Kogwa katika Kuenzi na Kuuendeleza Utamaduni wa Mswahili - *Mussa Mohamed Hans, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

Ushairi wa Kiswahili na Maendeleo ya Kenya tangu Uhuru - *Dkt. Edwin Masinde, Chuo Kikuu cha Kenyatta*

Utamaduni katika Tafsiri: Uchunguzi wa Mbinu za Kutafsiri Matini za Kiutamaduni za Kiswahili-Kiingereza - *Hadija Jilala, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania*

Miaka Hamsini ya “Leso” Mjini Mombasa: Kitambulisho cha Mswahili - *Dkt. Mwanakombo Mohamed, Chuo Kikuu cha Moi*

MJADALA

Jobo III (Chumba 02): Ufundishaji wa Kiswahili katika Nchi za Kigeni

Mwenyekiti: Dkt. Steven Elisamia Mrikaria

Utandawazi na Ufundishaji wa Kiswahili Ulimwenguni - *Mbwarali Kame, Chuo Kikuu cha Moi*

Ufundishaji wa Kiswahili Ughaibuni: Maendeleo na Changamoto - *Dkt. Kiarie Njogu, Chuo Kikuu cha Yale, Marekani*

Mwanafunzi wa Kigeni na Mkanganyiko wa Kiistilahi na Kisemantiki katika Kiswahili cha Tanzania Bara na Zanzibar - *Musa Mohamed Salim Shembilu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

Ufundishaji wa Kiswahili katika Nchi za Kigeni: Mfano wa Chuo cha Syracuse - *Dkt. Miriam Osore na Brenda Midika, Chuo Kikuu cha Kenyatta*

MJADALA

7.00 – 8.00 **MAAKULI**

8.00 – 10.00 **Shughuli za Majopo**

Jobo I (Ukumbi wa Mkuu): Matumaini ya Kiswahili Afrika na Ulimwenguni

Mwenyekiti: Prof. Sheila Ryanga

Ushairi wa Kiswahili na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki - *Dkt. Steven Elisamia Mrikaria, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

Kiswahili kama Chombo cha Maendeleo ya Usomi Ulimwenguni: Ufanisi na Changamoto - *Deborah Wanyama Amukowa, Chuo Kikuu cha Maseno*

Tafsiri na Uenezaji wa Kiswahili: Mifano kutoka Tamthilia za Stevene Kanumba - *Hadija Jilala, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania*

Usawiri wa Mwanamke katika Hadithi Fupi za Kiswahili. Mfano wa *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine* ya S.A. Mohamed - *Elizabeth K. Mue na Dkt. Edwin Masinde, Chuo Kikuu cha Kenyatta*

MJADALA

Jobo II (Chumba 01): Nafasi ya Kiswahili katika Ukombozi wa Wanawake

Mwenyekiti: Prof. Inyani Simala

Nafasi ya Kiswahili katika Ukombozi wa Wanawake - *Lina Akaka, Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki*

Fasihi Ekolojia Kifeministi: Taswira ya Marehemu Wangari Maathai katika Riwaya ya Nakuruto - *Dkt. Miriam Kenyani Osore na Aoko, Chuo Kikuu cha Kenyatta*

Hadithi Fupi kama Jahazi la Kumwoko Mwanamke - *Rose Mavisi na Florence Mũma, CUEA*

Miaka Hamsini ya Ujenzi wa Taswira ya Mwanamke katika Ushairi wa Kiswahili Nchini Kenya - *Prof. Clara Momanyi, Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki*

MJADALA

Jopo III (Chumba 02): Msamiati na Sera ya Lugha

Mwenyekiti: Dkt. Mbwarali Kame

Utamaduni-hamishwa Unavyodhihirika katika Msamiati wa Kiswahili - *Dkt. Iribe Mwangi, Chuo Kikuu cha Nairobi*

Maendeleo na Dosari katika Upanuzi wa Msamiati wa Kiswahili - *Prof. Rocha Chimera, Chuo Kikuu cha Pwani*

Utekelezaji wa Katiba: Mapendekezo ya Sera ya Lugha za Kenya - *Prof. Kimani Njogu, Twaweza Communications*

MJADALA

10.00 Ukumbi Mkuu
Matangazo: Kamati Andalizi

10.30 **CHAI**

ALHAMISI, TAREHE 22 AGOSTI

2.30 – 2.45 Ukumbi Mkuu
Mwenyekiti: Dkt. Mwenda Mukuthuria
Kurejelea Mijadala ya Siku ya Kwanza na Matangazo

2.45 – 3.30 *Mwenyekiti: Dkt. Mwanakombo Noordin*
Hotuba Maalum: Prof. Chacha Nyaigotti Chacha, CUEA
Mada: Maendeleo ya Miaka 50 ya Fasihi ya Kiswahili Nchini Kenya

3.30 – 5.00 **Shughuli za Majopo**

Jopo I (Ukumbi Mkuu): Kiswahili kama Nyenzo ya Maendeleo ya Uchumi wa Taifa

Mwenyekiti: John Marani

Kiswahili kama Lugha ya Mawasiliano katika Shughuli za Benki: Changamoto za Tafsiri - *Dkt. Jacktone Onyango, Chuo Kikuu cha Kenyatta*

Kiswahili kama Nyenzo ya Maendeleo ya Uchumi wa Taifa - *Jane Kanini Maithya, Chuo Kikuu cha Kenyatta*

Nafasi ya Kiswahili katika Utekelezaji wa Rajua 2030: Tathmini ya Kipindi cha Awali 2008 – 2012 - *Prof. Sheila Ali Ryanga, Chuo Kikuu cha Methodist-Bewa la Mombasa*

MJADALA

Jobo II (Chumba 01): Kiswahili, Uwiano wa Kitaifa na Utangamano

Mwenyekiti: Dkt. Edwin Masinde

Dhima ya Methali za Kiswahili katika Kuelimisha Jamii kuhusu Uwiano na Utangamano wa Kitaifa - *Dkt. Joseph Nyehita Maitaria, Chuo Kikuu cha Kenyatta*

Miziki ya Kiswahili kama Chombo cha Kuhimiza Swala la Uwajibikaji katika Jamii: Nyimbo za Baraka Mwinshehe - *Henry Indimuli, Chuo Kikuu cha Nairobi*

Kifanywe Nini Kiswahili ili Kifanye Nini? - *Dkt. Njoroge Ngugi*

MJADALA

Jobo III (Chumba 02): Kiswahili na Siasa

Mwenyekiti: Dkt. Kiarie Njogu

Jubilee ya “Mnazi Vuta N’kuvute”: Hali ya Kisiasa - *Alexander K. Rotich, Chuo Kikuu cha Kabianga*

Utambulisho wa Wanasiasa katika Diskosi za Kiswahili za Mihadhara ya Kisiasa (2012 – 2013) - *Dkt. Miriam Kenyani Osore, Chuo Kikuu cha Kenyatta*

Siasa za Lugha kama Mkakati wa Sera za Kisiasa katika Mdahalo wa Urais (Februari 2013) Nchini Kenya - *Dkt. Florence Ngesa Indede, Chuo Kikuu cha Maseno*

MJADALA

5.00 – 5.30 **CHAI**

5.30 – 7.00 Ukumbi Mkuu

Mwenyekiti: Dkt. Florence Indede

Wageni Maalum: Amina Vuzo, Jane Mumbua David, Daniel Watuha

Mada: Kiswahili katika Mitalaa ya Elimu

7.00 – 8.00 **MAAKULI**

8.00 – 10.00 Shughuli za Majopo

Jobo I (Ukumbi Mkuu): Utafiti wa Kiswahili: Lugha na Fasihi

Mwenyekiti: Prof. Isaac Ipara

Changamoto za Kujifunza Kirai Nomino cha Kiswahili Miongoni mwa Wanafunzi: Mchango wa Vitabu vya Kozi Vilivyoidhinishwa - *Leah Mwangi, Chacha Mwita na Dkt. Jacktone Onyango, Chuo Kikuu cha Kenyatta*

Utata wa Uainishaji Virai katika Mitalaa ya Shule za Upili Nchini Kenya - *Gladys Kinara, Pius Nyakundi na Dkt. Pamela Ngugi, Chuo Kikuu cha Kenyatta*

Najivunia kuwa Mkenya: Utosarufi, Mtindo au Mabadiliko ya Lugha? - *Dkt. Chacha Mwita, Chuo Kikuu cha Kenyatta*

MJADALA

Jopo II (Chumba 01): Utafiti wa Kiswahili: Lugha na Fasihi

Mwenyekiti: Prof. Peter Githinji

Maonyesho ya Urembo na Mitindo ya Mavazi: Fasihi ya Kisasa? - *Beth N. Mutugu, Chuo Kikuu cha Kenyatta*

Nadharia za Uhakiki kama Mchakato wa Kutaalamisha Usomaji wa Fasihi - *Dkt. Richard Wafula, Chuo Kikuu cha Kenyatta*

Miaka Hamsini ya Fasihi ya Kiswahili Nchini Kenya: Maendeleo, Changamoto na Mustakabali Wake - *Alex Umbima Kevogo, Chuo Kikuu Kishiriki cha Stella Maris, Tanzania*

MJADALA

Jopo III (Chumba 02): Utafiti wa Kiswahili: Lugha na Fasihi

Mwenyekiti: Mussa Mohamed Hans

Maudhui na Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za injili: Uchanganuzi wa Nyimbo za Rose Muhando - *Elizabeth K. Mue, Dkt. Edwin Masinde na Prof. G.K. King'ei, Chuo Kikuu cha Kenyatta*

Lugha Tamathali katika Habari za Soka: Mifano ya Matumizi katika Magazeti ya Kiswahili - *Kevogo Stanley Adika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Stella Maris Mtwara, Tanzania*

Makundi ya Lugha na Fasihi katika Facebook - *Rachel W. Maina, Chuo Kikuu cha Mount Kenya*

MJADALA

10.00 – 10.30 Ukumbi Mkuu
Matangazo: Kamati Andalizi

10.30 CHAI

IJUMAA, TAREHE 23 AGOSTI

2.30 – 3.30 *Mwenyekiti: Dkt. Miriam Osore*

Mada: Kiswahili na Uanahabari

Wawezeshaji: Prof. Ken Walibora (NMG), Leonard Mambo Mbotela (KBC), Mwanahamisi Hamadi (RMS)

3.30 – 5.00 **Shughuli za Majopo**

Jopo I (Ukumbi Mkuu): Kiswahili na Elimu

Mwenyekiti: Dkt. Richard Wafula

Tathmini ya Ufundishaji wa Kiswahili katika Vyuo vya Ualimu Nchini Kenya - *Rosemary A. Achillah, Chuo cha Ualimu cha Kamwenja*

Mchango wa Tume za Elimu Nchini Kenya katika Kukuza Lugha ya Kiswahili - *Gladys Kinara, Japheth Peter Muindu, Dkt. Edwin Masinde na Jackline Moraa, Chuo Kikuu cha Kenyatta*

Miaka Hamsini ya Maendeleo ya Kiswahili katika Elimu Nchini Kenya - *Prof. Isaac Ipara Odeo, Chuo Kikuu Kishiriki cha Kibabii*

MJADALA

Jopo II (Chumba 01): Utafiti wa Kiswahili: Lugha na Fasihi

Mwenyekiti: Khadija Jilala

Sheng na Kiswahili Sanifu: Rasilimali au Kiangamizi - *Prof. Peter Githinji, Chuo Kikuu cha Ohio, Marekani*

Je, Sheng ni lahaja ya Kiswahili? - *Dkt. Ayub Mukhwana, Chuo Kikuu cha Nairobi*

Mikondo katika Utafiti wa Isimu Nafsia - *Dkt. Mosol Kandagor na Salim Sawe, Chuo Kikuu cha Moi na Chuo Kikuu cha Kabianga*

MJADALA

Jopo III (Chumba 02): Kiswahili na Mwamko Mpya wa Afrika

Mwenyekiti: Dkt. Jacktone Onyango

Nafasi ya Kiswahili katika Demokrasia - *Beverlyne Asiko Ambuyo, Chuo Kikuu cha Maseno*

Tafsiri na Ufasiri katika Matumizi ya Kiswahili kama Lugha Rasmi Nchini Kenya - *Samson K. Nzyoka na Sarah Ngesu, Chuo Kikuu cha Kenyatta na Chuo Kikuu cha SEUKO*

Mustakabali wa Kiswahili na Maendeleo ya Jamii - *Prof. Inyani Simala, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro*

MJADALA

5.00 – 5.30 **CHAI**

5.30 – 6.15 *Mwenyekiti: Dkt. Mwanakombo Noordin*

Maamuzi na Mapendekezo

6.15 – 7.00 **UFUNGAJI**

Mwenyekiti: Prof. Clara Momanyi

Kufunga Kongamano: Prof. Justus Mbae, Naibu Makamu Mkuu (Taaluma) wa Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki

7.00 **MAAKULI**

IKISIRI

Mchango wa Redio na Runinga katika Makosa yanayofanywa na Wanafunzi katika Uandishi wa Insha

Daniel Kiprugut Ng'etich, Chuo Kikuu cha Kenyatta

Vyombo vya habari vimechangia pakubwa katika kuendeleza maisha ya binadamu. Usambazaji wa habari ulimwenguni umekuwa si jambo gumu tena. Hali hii imefanya ulimwengu kuwa kama kijiji kidogo. Kutokana na vipindi mbalimbali katika vyombo vya habari, wanajamii huathiriwa kwa namna moja au nyingine. Vijana ndio wanaoathiriwa kwa kiasi kikubwa kutokana na tabia yao ya kupenda kuiga mengi kutoka hasa kwa wale wanaowaona kuwa wa thamani kubwa kwao. Watangazaji, waigizaji na waratibu vipindi katika vyombo vya habari ni miongoni mwa watu wanaoathiri vijana kwa njia mbalimbali. Tatizo ni kwamba vijana hawa wakiwemo wanafunzi huiga masuala chanya na hasi. Hali hii imeathiri matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi kwa namna moja au nyingine.

Matumizi ya Kiswahili sanifu, hasa katika uandishi wa insha za Kiswahili, yameathirika kwa kiasi kikubwa. Kwa mujibu wa Gowon (2009), vyombo vya habari kama vile redio na runinga ni njia ya kuendeleza lugha katika jamii. Anaendelea kusema kuwa matumizi ya lugha katika vyombo vya habari huathiri matumizi ya lugha katika sekta ya elimu kihasi na kichanya. Makala haya yatabainisha jinsi lugha ya vyombo vya habari inavyoathiri uandishi wa insha miongoni mwa wanafunzi. Italenga kubainisha makosa mbalimbali yanayofanywa na wanafunzi wakati wa uandishi wa insha kutokana na athari za vyombo vya habari. Mifano itatolewa kutoka makosa yanayofanywa na baadhi ya wanafunzi kutoka Kaunti ya Baringo.

Dhima ya Methali za Kiswahili katika Kuelimishia Jamii kuhusu Uwiano na Utangamano wa Kitaifa

Joseph Nyehita Maitaria, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika, nyehitam@yahoo.com

Makala hii inabainisha nguvu ya methali katika kuipa nguvu lugha ya Kiswahili katika kuwaelekeza wanajamii kuzingatia uwiano na utangamano wa kitaifa nchini Kenya. Kwa hivi sasa, lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa lugha muhimu inayotuimika katika mawasiliano mapana ya watu; siyo tu nchini Kenya bali pia katika mataifa ya Afrika Mashariki na kwingineko. Katika mawasiliano hayo, wanajamii wamekuwa wakitumia kauli mahususi za kitamathali katika mawasiliano ya kijamii. Miongoni mwa kauli hizo ni methali ambazo zimekuwa zikitumika mno katika maingiliano hayo ya kijamii. Katika muktadha huo, lugha ya Kiswahili huwa ni chombo cha kuibulia na kuwasilisha falsafa inayohusu umuhimu wa kuzingatia uwiano na utangamano katika la Kenya. Mabadiliko mbalimbali ya kitamaduni, kijamii, kiuchumi nsa kisiasa yameweza kuutingisha mwafaka wa uwiano, utangamano na ushirikiano wa makundi tofauti tofauti yanayopatikana nchini humo hasa baada ya uhuru. Makala hii inafafanuliwa namna methali huipa nguvu lugha ya Kiswahili kuwa beramu ya kuzitafakarisha akili za watu kutambua umuhimu wa kuzingatia suala la uwiano na utangamano wa Wakenya ili kuepukana na mtazamo finyu wa kijamii. Kwa mfano, utamaduni wa watu uliokuwa ukishuhudiwa kabla ya miaka ya 1960 Afrika Mashariki (hasusan nchini Kenya), ni tofauti na ule wa baada ya uhuru hadi wakati wa sasa. Kupitia kwa methali zinazotumika katika mawasiliano hayo ya kijamii, ujumbe huo unaowasilishwa, hufasiriwa katika muktadha wa uelekezi wa vipengele vya utamaduni wa watu wa Kenya. Hiyo inamaanisha kuwa, nguvu ya matumizi hayo ya methali bado hayajapitwa na wakati. Matumizi hayo huipa nguvu lugha ya Kiwashili katika kusawazisha mwelekeo hasi wa ambao umekuwa ni kikwazo maendeleo ya jamii ya Wakenya kwa wakati wa sasa.

Changamoto za Kujifunza Kirai Nomino (KN) cha Kiswahili Miongoni mwa Wanafunzi: Mchango wa Vitabu vya Kozi Vilivyoidhinishwa

Leah W. Mwangi; Leonard Chacha na Jacktone Onyango, Shule ya Upili ya Passenga na Chuo Kikuu cha Kenyatta:
lemwangi2011@gmail.com, chachamwita8@gmail.com, tony60jacko@yahoo.com

Lugha ya Kiswahili nchini Kenya hufunzwa kama somo la lazima katika shule za msingi na za upili. Aidha, wanafunzi wengi wa Kiswahili wana lugha zao wenyeji na kwa hivyo hujifunza lugha hii kama lugha ya pili (L2). Ujifunzaji huu hutokea kupitia mifumo miwili mikuu: upataji lugha na ufunzaji rasmi unaofanyika darasani. Mafanikio katika ujifunzaji rasmi wa L2 huathiriwa na mambo kama vile: mbinu za kufunzia, vitabu vya kozi anavyotumia mwanafunzi, uwezo na hali ya kisaikolojia ya mwanafunzi. Utafiti huu ulilenga kutathmini mchango wa vitabu vya kozi katika ujifunzaji wa dhana hii ya kisarufi huku ikizingatiwa kuwa tafiti nyingi ambazo zimefanywa kuhusu dhana ya KN cha Kiswahili zilijikita katika kutathmini muundo na nafasi ya KN katika sentensi ya Kiswahili. Ni wazi kuwa vitabu vya kozi wanavyotumia wanafunzi kujifunzia dhana hii vina mchango mkubwa katika ama kuimarisha au kuzorotesha ufahamu wa mwanafunzi wa dhana ya KN. Baadhi ya athari hasi ambazo zilijitokeza kuhusiana na mchango wa vitabu hivi ni pamoja na: kushughulikia miundo michache sana ya KN, baadhi ya waandishi wa vitabu hivi walitoa mifano yenye makosa, huku wengine wakitoa mifano ya sentensi zilizoakisi miundo mbalimbali ya KN bila kumwelekeza mwanafunzi kuhusu ni miundo ipi iliyojitokeza katika sentensi walizotoa. Matatizo mengine ambayo yaliibuka kutokana na matumizi ya vitabu hivi ni: utungaji wa maswali machache na banifu, kutoshughulikia nafasi ya KN katika sentensi ya Kiswahili na kupendekeza njia zisizofaa zitumiwe na walimu kufunzia dhana hii. Utafiti huu ulifanywa kupitia upitiaji wa vitabu vya aina tatu vya kozi pamoja na nakala za wanafunzi waliochaguliwa kutoka shule tatu za upili Wilayani Nyandarua ya Kati ili kupata data iliyotumiwa kutoa mahitimisho ya utafiti huu.

Changamoto ya Tafsiri katika Simu za Rununu

John Marani, Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro: maranyke@yahoo.com

Simu za rununu hutekeleza jukumu kubwa la mawasiliano.hali hii hurahisisha mitagusano baina ya watu. Mawasiliano haya hupitia maongezi,jumbe fupi,twita na mitandao mingine.Simu hizi vile vile husaidia katika uhawilishi na usambazi wa pesa.Mashirika yanayomiliki simu hizi yanafanya juhudi kubwa za kuendeleza Kiswahili kwa kuitumia katika kueleza huduma muhimu wanazotoa kama vile:mpesa,pesa mkononi,M-kopa n.k.Ni jambo la kuvunja moyo kwa kuona mashirika haya yakitumia tafsiri isiyofaa. Tafsiri huwa ni muhimu kwa kuwa husaidia watu wasioelewa lugha asili kupokea ujumbe katika lugha pokezi. Ni muhimu hata hivyo kuzingatia tafsiri faafu ili kuufikisha uju namna ilivyokusudiwa.Tafsiri inapokuwa mbovu inaweza kupotosha ujumbe.Aidha, inaweza kuendelza lugha isiyo sanifu nahata kuathiri wanafunzi katika masomo yao na matokeo ya mitihani.Makala hii inajadili changamoto zinazojitokeza katika hizi. Inajadili tafsiri ambazo ni mbovu na kupendekeza tafsiri faafu inapowezekana.Tunatoa mifano kutoka mashirika ya Safaricom,Airtel na Orange.Tumeteua mashirika haya kutokana na idadi kubwa ya watumizi.Tunaangalia huduma tofauti zinazotolewa na mashirika haya ambazo zimetafsiriwa.Makala hii inapendekeza njia tofauti za kupunguza hali hii.Tuna imani kuwa mapendekezo haya yataweza kuwasaidia watawala wa mashirika kulipa suala la tafsiri uzito unaostahiki.Tafsiri itaendelezwa na watu ambao wa ujuzi wa taaluma ili siye ye yote anayethaniwa kuwa anaweza kuzungumza Kiswahili.

Jubilee ya ‘Mnazi Vuta N’kuvute’: Hali ya Kisiasa Nchini Kenya

Alexander K. Rotich, Chuo Kikuu Cha Kabianga: alexkipkemoi65@yahoo.com

Madhumuni ya makala hii ni kutathmini mivutano ya kisiasa nchini Kenya wakati nchi hii inapojiandaa kusheherekea miaka hamsini tangu ijipatie uhuru. Katika kufanya hivyo, makala itajikita katika vipindi vitatu muhimu vya kihistoria ambavyo ni miaka michache baada ya uhuru, miaka wa 2000 hadi 2013. Kulingana na kitabu kitakatifu cha Biblia, mwaka wa hamsini katika jamii ya Wayahudi ulikuwa muhimu sana. Hii ni kwa sababu, taifa ilipofikisha miaka hamsini mambo mengi mazuri yalitukia. Baadhi ya mambo hayo yalikuwa pamoja na watumwa kuachiliwa huru, wanyanganyi kurejesha mali ya umma walionyakua na hivyo kila myahudi kupata haki yake. Mwaka wa jubilee kama ulivyokuja kujulikana, ulitarajiwa na wengi waliokuwa wamenyimwa haki zao. Walingojea mwaka wa jubilee wakiwa na hisia za matumaini makubwa sana. Nchini Kenya, wakati wa kampeini za uchaguzi mwaka wa 2012, neno jubilee lilitumiwa sana mirengo miwili mikuu ya kisiasa iliyokuwa ikishindania uongozi katika muktadha huu, kila mrengo ulitumia neno hili kujipigia debe. Neno ‘Jubilee’ likawa linavutwa pande mbili za kisiasa kila mrengo ukivuta kuelekea upande wake jinsi afanyavyo kila mwamba ngoma. Katika mvutano wa hivi karibuni wahusika wakuu walikuwa vibwana wa wahusika wakuu katika mvutano wa awali ambao nao wanawakilishwa na Ali na Badi katika Shairi la Abdilatif Abdallah “Mnazi Vuta N’kuvute”. Licha ya mvutano ulikuwepo, kumekuwa na ufanisi katika nyanja mbalimbali. Huu ni ufanisi ambao taifa linajiandaa kuusherekea kwa mbwembwe na taadhima za aina yake. Tunaposherehekea mwaka wetu wa Jubilee basi, inatupasa tujiulize; Je, Yule ndugu aliyekuwa juu mnazini ameshuka ili kumpisha nduguye naye au faidi mnazi? Je, wote wawili wako juu mnazini? Au wote wawili wako chini ya mnazi. Haya ni baadhi ya maswali ambayo makala hii itajaribu kuyajibu.

Kiswahili kama Lugha ya Mawasiliano katika Shughuli za Benki: Changamoto za Tafsiri

Jacktone O. Onyango, Chuo Kikuu cha Kenyatta: tony60jacko@yahoo.com

Lugha ya Kiswahili imechangia pakubwa katika kuleta maendeleo ya uchumi wa taifa la Kenya. Ni lugha inayotumiwa kufanikisha mawasiliano ya kibiashara katika sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na sekta ya huduma za benki. Hata hivyo, licha ya Kiswahili kuwa lugha rasmi ya taifa, bado haitumiwi kikamilifu katika utoaji wa huduma za benki. Sababu mojawapo inayochangia hali hii ni kwamba kuna changamoto za kutafsiri kwa Kiswahili baadhi ya istilahi zinazotumiwa kuendesha shughuli za benki. Kwa misingi hiyo, makala hii inalenga kuchunguza istilahi zinazotumiwa katika mawasiliano ya benki na changamoto za kutafsiri istilahi hizo kwa Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yatachangia kuimarisha matumizi ya Kiswahili katika shughuli za benki kutokana na uundaji wa istilahi zinazofaa kufanikisha mawasiliano. Istilahi hizo zinaweza kutumiwa katika mawasiliano ya ana kwa ana, uandishi wa stakabadhi za benki na utoaji wa huduma za benki mtandaoni. Istilahi hizo pia zinaweza kuchapishwa katika kamusi ya kitaaluma ambayo itachangia kuziba pengo la marejeleo ya kileksikografia. Kwa kufanya hivyo, watu wengi wataweza kufikiwa na huduma za benki na hivyo basi kuchangia kuleta maendeleo ya uchumi wa taifa.

Kiswahili kama Nyenzo ya Maendeleo ya Uchumi wa Taifa

Jane Kanini Maithya, Chuo Kikuu cha Kenyatta

Kiswahili ni mojawapo wa lugha za kiasili nchini Kenya. Asili yake ni Pwani ya Kenya. Ni lugha ambayo imeenea kwa kasi barani Afrika na hata duniani kote. Nchini Kenya na Tanzania, Kiswahili ni lugha rasmi na ya kitaifa. Kiswahili ni lugha ya pekee yenye uwezo wa kutumika kama “Lingua Franca” ya bara hili (Buliba, 2001). Kutokana na kuenea kwake, lugha ya Kiswahili ni nyenzo muhimu ya kuiendeleza nchi kiuchumi.

Hutumika kuendeleza shughuli za biashara kitaifa na kimataifa, kuendeleza kilimo, waimbaji huitumia kujichumia riziki na kadhalika. Kulingana na Djite (1993), lugha ambazo zitaendeleza Afrika na kuleta mabadiliko ya kiuchumi ni lugha za kiafrika na wala si za kigeni. Kiswahili basi kina nafasi bora zaidi ya kutekeleza jukumu la kuendeleza taifa kiuchumi kwani ni lugha ya Kiafrika inayotumiwa na watu wa matabaka yote katika shughuli za kisiasa na kiuchumi. Utafiti huu utajibu maswali: Je, Kiswahili kina mchango gani katika kuendeleza uchumi wa taifa? Kina sifa gani zinazokiwezesha kutekeleza jukumu hilo? Kuna changamoto zozote zinazokikumba Kiswahili katika utekelezaji wa jukumu hilo? Makala hii itawafaa sana waundaji wa sera ya lugha nchini.

Nafasi ya Kiswahili katika Demokrasia

Beverlyne Asiko Ambuyo, Chuo Kikuu cha Maseno

Demokrasia ni aina ya siasa ambayo husisitiza zaidi ushirikiano na maelewano katika kuendesha shughuli mbalimbali za kijamii. Wataalamu mbalimbali wameeleza ya kwamba siasa ya kidemokrasia ni siasa inayoendeshwa katika lugha ya kienyeji. Hili linamaanisha kuwa si rahisi kupata siasa ya kidemokrasia katika jamii yenye wingi lugha katika viwango vya kieneo, kitaifa na hata kimataifa. Kazi hii ina lengo la kueleza namna ambavyo siasa za kidemokrasia huendeshwa kupitia lugha. Hili litashughulikiwa kwa machukulio kuwa siasa za kidemokrasia ni zile ambazo kila mshirika anajitahidi kuelewa, kutangamana na kuwashirikisha watu wote katika maamuzi muhimu kuwahu. Masuala ya demokrasia nchini Kenya na hata eneo la Afrika Mashariki yameshika kani katika taasisi zote za kijamii. Mikakati mbalimbali imewekwa katika taasisi hizi kuhakikisha kwamba utangamano mzuri unaendelezwa kwa minajili ya kuleta maendeleo hasa kwa kuzingatia malengo ya milenia na ruwaza ya mwaka 2030. Inavyobainika lugha ya Kiswahili ina jukumu la kuendeleza utangamano miongoni mwa watu wa jamii na maeneo mbalimbali. Hivyo basi lugha hii ina nafasi kubwa katika maendeleo ya demokrasia sio tu nchini Kenya au Afrika Mashariki bali ulimwenguni kote.

Maonyesho ya Urembo na Mitindo ya Mavazi: Fasihi ya Kisasa?

Beth N. Mutugu, Chuo Kikuu cha Kenyatta

Katika siku za hivi karibuni hasa katika karne hii, ulimwengu umeshuhudia tamasha za urembo na mitindo ya mavazi mbalimbali ambazo zimekuwa zikiandaliwa mahsusi kote ulimwenguni. Tamasha hizi huwa na malengo mbalimbali ambayo hutimizwa kupitia kwa wahusika ambao hujitokeza na kuonyesha mitindo mbalimbali ya mavazi na miondoko mbalimbali. Zaidi ya haya, urembo wa wahusika hawa huwa ni kigezo maalum na muhimu cha kuamua ufanisi wao katika maonyesho haya. Watu wengi wanatazama maonyesho haya kama mojawapo ya athari za kigeni ambazo zimeikumba Afrika na kwamba ni jambo linalohusishwa na watu wanaoishi mijini. Hata hivyo tukiangalia tamasha hizi kwa jicho pevu, tunaweza kuona vipengele vingi vya fasihi simulizi ambavyo vinashirikishwa. Fasihi simulizi ina sifa zake mahsusi ambazo hujidhihirisha katika tanzu zake mbalimbali. Baadhi ya sifa hizi ni utendaji, hadhira, wahusika, ubunifu na kadhalika.

Fasihi simulizi inakabiliwa na changamoto mbalimbali hasa kutokana na maendeleo na mabadiliko ya kijamii katika nyanja tofauti. Hata hivyo, ni wazi kuwa bado kuna mambo mbalimbali yanayofanyika katika ulimwengu wa sasa yanayoshirikisha vipengele vya fasihi simulizi. Lengo la makala hii ni kujadili ni kwa jinsi gani fasihi simulizi ya jadi inawakilishwa katika maonyesho ya urembo na mitindo ya mavazi ya kisasa na ni kwa jinsi gani yanavyojumulisha hali halisi ya ulimwengu wa sasa.

Matumizi ya Tarakalishi katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili Nchini Kenya

Florence A. Miima na Rose M. Mavisi na Vincent F. Kawoya, Chuo Kikuu cha Kenyatta na Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki

Tarakilishi ni mojawapo ya nyenzo zinazohimizwa kutumiwa katika kurahisisha uelewa wa mwanafunzi katika viwango vyote vya elimu ulimwenguni, Kenya ikiwemo. Nchini Kenya, serikali na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali yanafanya juhudi kusamabaza na kuongeza idadi ya tarakilishi katika baadhi ya shule ili kutumiwa kama nyenzo katika ufundishaji na ujifunzaji wa masomo mabalimbali yanayofundishwa shuleni, lugha ya Kiswahili ikiwemo. Kiswahili ni lugha ya taifa, rasmi na inatambuliwa kote ulimwenguni. Kwa hivyo, inatarajiwa kufundishwa kwa kutilia maanani teknolojia ya kisasa ili kufikia malengo ya Milenia na ruwaza ya 2030. Makala hii inalenga kuweka wazi namna tarakilishi inavyoweza kushirikishwa katika kufunza na kujifunza Kiswahili katika shule za upili. Makala vile vile yatatalii changamoto zinazoweza kutokea katika mchakato wa matumizi ya tarakilishi.

Nadharia za Uhakiki kama Mchakato wa Kutaalamisha Usomaji wa Fasihi

Richard M. Wafula, Chuo Kikuu cha Kenyatta

Uandishi na usomaji wa Fasihi ya Kiswahili umepanuka sana katika miongo mitano iliyopita. Makala haya yanauia kuonyesha dhima ya nadharia katika kutaalamisha usomaji wa fasihi. Nadharia za uhakiki (na wakati mwingine za utunzi) zimepevusha usomaji na uhakiki kwa viwango ambavyo havingeweza kukadirika hapo awali. Kwa njia hii, lugha ya Kiswahili imeweza kueleza maarifa anuwai kwa viwango vya juu. Nadharia na mikondo ya uhakiki kama usemezano na Udenguzi imetuwzesha kuchanganua matini ya kifasihi kwa jicho la upekuzi. Kwa upande mwingine, changamoto kuhusiana utumiaji wa baadhi ya hizi nadharia zimezuka na zinapaswa kutathminiwa katika mazingira ambamo lugha ya Kiswahili inaendelea kutumiwa kufafanulia ujuzi wowote ule.

Nafasi ya Kiswahili katika Ukombozi wa Wanawake

Lina Akaka, Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki

Karatasi hii itautathmini uwezo wa lugha ya Kiswahili kama kifaa cha ukombozi wa wanawake katika nyanja zote za maisha. Ni jambo la kusikitisha kuwa wanawake wengi hususan wa mashinani hawajakombolewa kimawazo, kiuchumi, kisheria, kisiasa, kidini na kijamii kwa sababu ya mipaka ya kiisimu mbali na ya kielimu. Mipaka ya kiisimu inaweza kuwa njia mojawapo ya kutowahusisha wananchi katika shughuli za kiuchumi na kisiasa kikamilifu, Bamgbose (2000). Ni kwa misingi hii, ambapo karatasi hii itachunguza jinsi lugha ya Kiswahili inavyoweza kutumiwa kama kifaa cha ukombozi wa wanawake. Nadharia ya ufeministi itatumiwa kuiongoza kazi hii.

Vuguvugu la harakati za ukombozi wa wanawake lilishuhudiwa katika nchi za kimagharibi katika karne ya kumi na tisa. Mifumo ya kibabedume iliyojengeka kwenye misimamo na itikadi ya kiume iliwakandamiza wanawake kidini, kiuchumi, kisaikolojia na kisanaa. Kwa kuwa elimu na uchumi una uhusiano wa karibu mno katika mataifa yaliyoendelea, mifumo hii ya kibabedume haikuwaruhusu wanawake kuwa na elimu ya juu, Millet (1978). Kupitia mpito wa wakati, harakati za ukombozi wa wanawake zilichukua sura mbalimbali kila mojawapo ikiangazia vigezo tofauti na nyingine kutegemea ukandamizwaji uliofanyiwa wanawake katika maeneo mbalimbali duniani, Ramazanoglu (1989). Hali hii ilizaa matapo mbalimbali ya ufeministi, Wafula na Njogu (2007).

Kenya haikuachwa nyuma katika juhudi za ukombozi wa wanawake. Kuanzia miaka ya themanini waandishi wa fasihi ya Kiswahili walishughulikia swala hili katika tanzu zote za fasihi. Kwa upande ule mwingine, mashirika yasiyo ya kiserikali pamoja na serikali ilianzisha kampeni za kumwinua mwanamke kielimu, kiuchumi na kisiasa. Lugha ya Kiswahili ndiyo iliyotumiwa katika uzinduaji, uhamasishaji, uwezeshwaji na ukombozi wa wanawake mashinani na mijini kwani anavyosema Edwards (1976) kuwa lugha inayotimiza mahitaji ya jamii kimawasiliano ndiyo inayokuwa chombo muhimu katika ujenzi wa taifa.

Nafasi ya Mwaka Kogwa katika Kuuenzi na Kuuendeleza Utamaduni wa Mswahili

Mussa Mohamed Hans, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili- Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Jamii yoyote iwayo duniani huwa na utamaduni wake ambao aghalabu hutumika katika kuitofautisha jamii hiyo na jamii nyingine, za karibu au za mbali. Ingawa kumekuwa na mjadala mpana na endelevu kuhusu dhana ya Mswahili, wanazuoni wengi wanakubaliana kwamba chimbuko la Kiswahili ni upwa wa Afrika Mashariki. Ni katika maeneo haya pia ndimo mnamopatikana lahaja nyingi za Kiswahili. Hivyo, utamaduni wa jamii pana ya Waswahili unaweza kupatikana kupitia katika jamii ndogondogo za wazungumzaji wa lahaja hizi. Makunduchi ni miongoni mwa maeneo yanamozungumzwa lahaja za Kiswahili. Lahaja inayozungumzwa katika eneo hili inaitwa Kimakunduchi.¹ Miongoni mwa matukio muhimu ya kijadi yanayofanyika katika jamii ya Wamakunduchi ni sherehe za Mwaka Kogwa. Kwa Wamakunduchi hii ni sherehe kubwa kuliko sherehe nyingine yoyote inayofanyika katika jamii hii. Wamakunduchi kutoka sehemu mbalimbali hukusanyika katika uwanja wa Mwaka Kogwa ili kutekeleza jadi yao. Sherehe hizi pia huhudhuriwa na watu mbalimbali kutoka kila kona ya dunia.

Lengo la makala haya ni kubainisha nafasi ya sherehe za Mwaka Kogwa katika kuuenzi na kuendeleza utamaduni wa Mswahili. Makala yataanza kwa kutoa maelezo ya jumla kuhusu dhana ya Mwaka Kogwa na kisha kujadili nafasi yake katika kuuenzi utamaduni wa Mswahili. Makala yatajadili pia changamoto mbalimbali zinazozikabili sherehe za Mwaka Kogwa na kutoa mapendekezo ya nini kifanyike ili kukabiliana na changamoto hizo.

Mchango wa Vyombo vya Habari katika Maendeleo ya Kiswahili: Mfano wa Gazeti la Taifa Leo

Ngugi Kariuki na Ontieri Omari, Chuo Kikuu cha Masai Mara

Vyombo vya habari ni asasi muhimu katika uenezaji wa lugha ya Kiswahili katika karne ya 21. Vyombo hivi vya habari ni pamoja na: Redio, runinga na magazeti. Waandishi wa habari wamejizatiti kupasha habari kwa kutumia lugha sanifu ya kiswahili. Jambo hili limesahilisha mawasiliano na kuwawezesha watu wengi kufikiwa na habari muhimu za kitaifa na kimataifa. Kazi hii imelenga kuchunguza mchango wa vyombo vya habari, hususani gazeti la Taifa Leo katika kustawisha na kuendeleza lugha ya kiswahili. Utafiti huu umetumia mbinu ya uchanganuzi matini. Gazeti la Taifa Leo, huwa na makala anuwai yanayohusu lugha na matumizi yake. Baadhi yao huwa ni vibonzo, chemshabongo pamoja na methali. Makala kama yale ya ufasaha wa lugha na fasihi, yameangazwa. Mambo haya hukuza uwezo wa wasomaji wa kutumia na kukuza Kiswahili. Makala haya yanatarajiwa kutoa mchango mkubwa kwa watafiti wa baadaye kuhusu nafasi ya vyombo vya habari katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Aidha, kwa waandishi wa habari, makala haya yataelekeza kuhusu njia bora zaidi za kutumia vyombo vyao katika kukuza lugha ya Kiswahili ambayo ndiyo lugha rasmi na taifa nchini Kenya; lugha ya taifa nchini Tanzania na lugha ya matumizi mapana katika ukanda wa Mashariki mwa Afrika.

¹ Lahaja hii hujulikana pia kwa jina la Kikae. Katika baadhi ya maandiko ya zamani jina lililotumika sana ni Kihadimu. Hata hivyo jina la Kihadimu kwa sasa halitumiki sana kwa kuwa linanasibishwa na utumwa.

Tafsiri na Ufasiri katika Matumizi ya Kiswahili kama Lugha Rasmi Nchini Kenya

Samson K. Nzyoka, Chuo Kikuu cha Kenyatta: kigospeli@gmail.com

na

Sarah Ngesu, Chuo Kikuu cha SEUKO: sarahngesu@gmail.com

Safari ya Lugha ya Kiswahili ya kufikia kiwango cha kupata hadhi ya kuwa lugha rasmi kikatiba katika nchi yetu ya Kenya imekuwa ndefu na yenye changamoto nyingi. Katiba mpya ya Kenya iliyoidhinishwa mwaka 2010 imepatia lugha ya Kiswahili nafasi ya kuwa lugha rasmi. kwa sasa ni miaka 50 tangu nchi yetu ilipoupata uhuru wa bendera kutoka kwa wabeberu. Tunaposherehekea Mwaka huu wa 2013 wa Jubilee, wapenzi wa Kiswahili wanalo jambo la kufurahia, nalo ni hili la Kiswahili kuwa lugha rasmi. Katika sura ya pili ibara ya 7(1) inakariri kuwa lugha ya taifa ya jamuhuri ya Kenya ni Kiswahili. Ibara ya pili inasema lugha rasmi za jamuhuri ya Kenya ni Kiswahili na Kiingereza. Makala hii inalenga kubainisha hali ilivyo kwa sasa katika matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi baada ya kuidhinishwa kikatiba nchini Kenya. Aidha inalenga pia kuonyesha nafasi ya ufasiri na tafsiri katika utekelezaji wa wajibu huu wa kikatiba. Nafasi ya lugha ya Kiingereza kikatiba ni sawa na lugha ya Kiswahili katika matumizi rasmi. Maswali ambayo, wataalamu na wapenzi wa lugha hii wanayoweza kujiuliza ni; Je, baada ya katiba ya Kenya kukifanya Kiswahili kuwa lugha rasmi, hali ya matumizi ya lugha hii imefika wapi?, Je lugha hii, ina uwezo wa kutekeleza majukumu yanayotekelezwa na Kiingereza kama lugha rasmi_mwenza?, Swali jingine muhimu ni; je ufasiri na tafsiri zinaweza kuchangia vipi katika matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi?. Matumizi ya lugha hii imebainishwa katika idara mbalimbali kama mahakama, mijadala ya bunge, hotuba za viongozi watawala, katika vyombo vya habari, hospitalini, uzambazaji na uuzaji wa magazeti miongoni mwa asasi na maeneo mengine ya umma.

Tathmini ya Ufundishaji wa Kiswahili katika Vyuo vya Ualimu Nchini Kenya

Rosemary A. Achillah, Chuo cha Ualimu cha Kamwenja

Makala hii inajadili upeo, mbinu na changamoto za ufundishaji wa Kiswahili katika vyuo vya ualimu nchini Kenya. Mwandishi anahoji kuwa kuna mikakati mbalimbali ambayo inaweza kuchangia katika kuimarisha viwango vya ufundishaji huo.

Najivunia Kuwa Mkenya: Utosarufi, Mtindo au Mabadiliko ya Lugha?

Chacha Mwita, Chuo Kikuu cha Kenyatta: chachamwita8@ygmail.com

Makala haya yanazungumzia dhima ya kiambishi cha kauli ya kutendea ya kitenzi cha Kiswahili huku ikirejelea sentensi mbili (a) “Najivunia kuwa Mkenya” na (b) “Navumilia kuwa Mkenya”. Usarufi na utosarufi wa kauli hizo unazungumziwa. Mitazamo miwili ya lugha inatumiwa: mtazamo elekezi na mtazamo elezi. Katika kiwango cha mtazamo elekezi, makala yanaonyesha utosarufi uliomo katika sentensi “Najivunia kuwa Mkenya”; na katika kiwango cha mtazamo elezi wa lugha, makala yanachambua matumizi mengineyo ya kiambishi hicho cha kutendea.

Ushairi wa Kiswahili na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki

Steven Elisamia Mrikaria, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: imrikaria@hotmail.com

Kwa mujibu wa Shaaban Robert (1968) ushairi ni sanaa ya vina, yenye ufasaha wa maneno machache au muhutasari wa mawazo, maono na fikra za ndani zinapoelezwa kwa muhutasari, huvuta moyo kwa namna ya ajabu. Maneno hayo ya S. Robert yanatuvuta kuangalia namna wataalamu wetu wa Ushairi wa Kiswahili walivyotumia dhana na mitazamo yao kuuangalia utanzu huu wa fasihi.

Katika kuyachambua na kuyanyumbua hayo, tutaangalia jinsi ushairi wa Kiswahili unavyoangaliwa hivi kuwavutia wanajumuiya muruwa wa shirikisho la Afrika ya Mashariki (A. Mashariki). Lengo letu katika makala haya ni kuibua mjadala wa kutumia maneno ya hekima kuibua na kuimarisha kwa kuendeleza na kuitangaza jumuiya hii. Mwisho wa mjadala wetu, tutaibua mbinu na nadharia mbalimbali zitakazotusaidia kuenzi Ushairi wa Kiswahili ndani na nje ya A. Mashariki.

Utambulisho wa Wanasiasa wa Kenya katika Diskosi za Kiswahili za Mihadhara ya Kisiasa za Mwaka 2012-2013

Miriam Kenyani Osore, Chuo Kikuu cha Kenyatta

Suala la wanasiasa na diskosi za kisiasa ni mojawapo kati ya maswala ambayo huangaziwa na vyombo vya habari humu nchini na hata sehemu zingine ulimwenguni. Baadhi ya haya maswala yanayoangaziwa ni kama vile lugha ya kisiasa, uchanganuzi wa kisiasa na utambulisho wa kisiasa. Humu nchini Kenya, wanasiasa wengi wanapojipigia debe na kunadi sera zao za kisiasa aghalabu hujitambulisha na wapiga kura kwa lengo la kuwashawishi ili wawapigie kura. Utambulisho huu mara nyingi hujadiliwa na hao wananchi na huathiri mielekeo yao ya kisiasa na jinsi wanavyowasawiri hao wanasiasa na vyama vya kisiasa. Hii hupelekea mivutano na kutokuwa na amani miongoni mwa wanachi hivyo nchi nzima kuegemea upande wa ukabila au mapendeleo yasiyo na tija kwa mustakabali wa taifa na utangamano wa kijamii, udunishaji wa utamaduni, na mizozano ya kidini. Mara nyingi wanasiasa hawa huzungumza diskosi zao bila ukweli, bila utaifa, bila uzalendo na bila kuwa dhiti na kile ambacho wanajitambulisha kwacho na ndio mambo ambayo hupelekea kuzuka kwa matatizo hayo. Baadhi ya wananchi huishia kuwapigia kura na baadaye kujutia wakati wanasiasa hao wanapobatili diskosi zao wakiwa madarakani. Utafiti huu kwa hivyo unapania kuchanganua diskosi hizi za wanasiasa katika vyombo vya habari, hasa kwa kuchanganua kanda mbalimbali za video zilizochukuliwa na wanahabari wakati wa kampeni nchini Kenya. Utafiti huu unalenga kujadili kwa utondoti aina za utambulisho ambazo wanasiasa hutumia katika kampeni zao na pia kujadili dhima, na muktadha wa diskosi hizi za utambulisho.

Fasihi Ekolojia Kifeministi: Taswira ya Marehemu Wangari Maathai katika Riwaya ya Nakuruto

Miriam Kenyani Osore na Aoko, Chuo Kikuu cha Kenyatta

Ekolojia yetu imo katika hatari ya kuangamizwa kutokana na matendo ya kibinafsi ya kibinadamu. Matendo kama vile kukata miti, kujenga nyumba katika maeneo oevu, kuongezeka kwa teknolojia haribifu na ukosefu wa uongozi adilifu katika suala la mazingira yamesababisha mitandao ya viungauhai kudhoofika. Mwisho wa matendo haya ni kwamba jotohewa limeongezeka na kuvuguta sayari yetu, magonjwa yamezidi, vifo vimekithiri, na mazao katika jamii zetu yamepungua hivyo kusababisha njaa. Athari hizi zinatatiza maisha ya binadamu na maendeleo endelevu kiuchumi. Miaka ya hivi karibuni, wataalam wa angahewa, mazingira na pia wanaharakati wamejitokeza kuzindua wanadamu wote katika sayari ya leo kuhusu tata za kiekolojia zinazomkabili mwanadamu.

Badhi ya wanaharakati hawa ni kama vile watunzi wa riwaya za Kiswahili. Watunzi hawa kama vile Said Ahmed Mohamed na Clara Momanyi na mtunzi wa Bustani ya Edeni wameonyesha kwamba riwaya ina mchango mkubwa katika upashaji wa ujumbe wa kimazingira. Hata hivyo kila mtunzi ana mtazamo wake wa kiekolojia na jinsi ya kuukabili. Mtunzi wa Nakuruto ameonyesha kwamba nafasi ya mwanamke katika utunzaji wa mazingira ni kubwa na haifai kupuuzwa. Kwa kujadili (kifeministi) riwaya ya Nakuruto, tutaonyesha kwamba msanii Clara Momanyi alikuwa na taswira ya matendo ya Marehemu Wangari Maathai na kwamba utunzi wake ulichukua mwelekeo wa kifeministi. Tutaonyesha kwamba maisha ya Mhusika Mkuu wa Nakuruto ni picha halisi ya harakati za marehemu Maathai.

Hadithi Fupi kama Jahazi la Kumkomboa Mwanamke

Rose Mavisi , Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki: rosemasai@gmail.com

na

Florence Miima, Chuo Kikuu cha Kenyatta: Miimaflo@yahoo.com

Suala la mwanamke limekuwa la mjadala muhimu katika karne hii . Suala la ukombozi wa mwanamke lilianza kutiliwa maanani kupitia fasihi ya Kiswahili miaka ya themanini. Hadi wa leo waandishi wengi wametumia kazi zao kama jukwaa la kumkomboa mwanamke. Wametamba kupitia riwaya, tamthilia, ushairi na hata hadithi fupi.

Katika makala haya tunanua kuweka wazi juhudi za waandishi wa hadithi fupi kutumia kazi zao kama jahazi la kumkomboa mwanamke. Makala haya yatalenga hadithi fupi mbili kutoka diwani ya Mayai Waziri wa Maradhi nazo ni Uteuzi wa moyoni yake Rayya Timamy na Ngome ya nafsi yake Clara Momanyi. Tutajaribu kuzitalii ili tuweze kuonyesha jinsi zinamsaidia mwanamke kujikomboa. Nadharia ya ufeministi kitengo cha Unisai wa kiasia itatumika ili kuweza kuweka wazi suala hili. Hii nadharia inayotaribu kuchunguza na kutatua matatizo yanayowakabili wanawake. Hawa wanawake wamekuwa wakipigania haki zao katika kipindi chote ambacho binadamu ameishi katika sayari hii.

Utandawazi na ufundishaji wa Kiswahili kwenye ulimwengu

Mbwarali Kame, Chuo Kikuu cha Moi: dktabuyaasir@gmail.com

Tunapo angalia ulimwengu wa sasa twapata yakuwa kuna mengi ambayo yameibuka na hasa kwenye suala la mawasiliano na Utandawazi, ni hivi majuzi tu ambapo suala la utandawazi lilijadiliwa kwa kina kwenye makongamano tafauti na ikawa suala la lugha niigezo kikubwa cha kujadiliwa kwenye makongamano kama hayo. Kwa hakika lugha ndio kioo muhimu kwenye ulimwengu wa utandawazi ni lugha nyingi zimewekwa kwenye kila chombo kinacho shughulikia utandawazi kwenye ulimwengu kama huu. Kiswahili ni lugha pana sio kwa nchi za Africa Mashariki bali kwa ulimwengu mzima ni lugha iliyo tambulika na wengi na hata kuingizwa lugha ya Kiswahili kwenye tarakilishi mbali mbali na kwenye mitandao. Katika makala haya tutajadili suala la utandawazi na kuchunguza dhana ya utandawazi wenyewe kwenye dunia hii ya sasa, pamoja na kuchunguza kwa kina namna ya lugha ya Kiswahili ilivyo tumika na sasa inavyo tumika kwenye suala la utandawazi, pia namna utandawazi ulivyo ikuza lugha ya Kiswahili na maendeleo yanayo tarajiwa kwa lugha ya Kiswahili kwa kuibuka mifumo ya utandawazi kwenye ulimwengu kama huu. Pia tutaangazia lugha ya Kiswahili namanuafaa katika taaluma, na jamii na uchumi kwa utangulizi huu nafikiri itakuwa nimefikia malengo ya kongamano la CHAKITA.

Kiswahili kama Chombo cha Maendeleo ya Usomi Ulimwenguni: Ufanisi na Changamoto

Deborah Nanyama Amukowa, Chuo Kikuu Cha Maseno

Lugha huwapanulia wanadamu nafasi ya kutekeleza mambo kadha wa kadha. Isitoshe, huakisi kiwango na aina ya mawazo ambayo huzalishwa na wanajamii. Hivyo basi, lugha humwezesha mwanajamii kueleza mawazo yake kwa namna ambayo inafaa. Aghalabu binadamu hujifunza namna ya kufikiria kabla ya kujifunza kujieleza kupitia lugha. Kiwango cha thamani na hadhi ya lugha ni kama kipima-joto cha afya razini ya watu. Lugha basi ina uhusiano wa karibu na utambulisho wa watu katika jamii maalum. Kupitia hili, lugha hutimiza majukumu muhimu kutokana na juhudi za kuchangia utimizaji wa mawasiliano miongoni mwa wanadamu. Lugha hutimiza majukumu ya kuwa chombo, nyenzo na chanzo cha mantiki yaliyomo katika mawasiliano yoyote ikiwemo michakato ya kiusomi au kiakademia. Makala hii inajadili namna ambavyo mielekeo na maendeleo ya Kiswahili imeweza kunaswa katika mkondo wa kiakademia/ kiusomi kiutandawazi.

Ushairi wa Kiswahili na Maendeleo ya Kenya tangu Uhuru

Edwin Masinde, Chuo Kikuu cha Kenyatta

Kazi hii inajaribu kubainisha kwamba lugha ni nguzo muhimu katika mawasiliano ya jamii. Ni chombo muhimu kinachoongoza mienendo ya watu katika jamii. Huwawezesha watu kuingiliana na kuathiriana. Hivyo, mawasiliano baina ya wanajamii ni muhimu na ya kimsingi kwa ufanisi wowote. Ni nguzo kuu ya kila kinachoweza kufanyika na vile kinavyoweza kufanyika kwa sababu huweza kuwawekea watu mipaka kuhusu yale wanayoweza kufanya. Lugha inayotumiwa na wanajamii na ambayo wanaielewa huathiri namna wanavyojifikiria, kutenda na nafasi yao katika jamii yao. Aidha, kazi hii inaonyesha kwamba fasihi ya Kiswahili, hususa, ushairi umetekeleza wajibu muhimu katika maendeleo ya miaka 50 ya uhuru. Ushairi umekuwa ukiwatazamisha wanajamii mazingira yao wakayaona, ukawaadilisha, kuwazindua, kuwatahadharisha, kuwakejeli, kuwaongoza, kuwasifu na kadhalika.

Maudhui na Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Injili; Uchanganuzi wa Nyimbo za Rose Muhando

Elizabeth k. Mue, E.W. Masinde na G.K.King'ei, Chuo Kikuu cha Kenyatta: elizabethkasau@gmail.com

Makala hii inakusudia kubainisha ukuaji na kuendelea kwa lugha ya Kiswahili katika uwanja wa muziki wa injili. Tangu mataifa ya Afrika Mashariki yachukue uhuru kutoka kwa mkoloni, kuna mataifa ambayo yameendelea na kukuza lugha ya Kiswahili hadi kufikia upeo wa juu. Mfano mzuri wa mataifa kama haya ni jirani zetu Tanzania. Lugha ya Kiswahili ilipewa nafasi ya kukua na mwalimu Juliasi Nyerere. Kwa sasa lugha ya Kiswahili imekua kwa kiwango kikubwa nchini Tanzania. Waimbaji wa kutoka taifa hili wameendeleza matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu. Rose Muhando anaweza kuwa mfano mzuri wa kuigwa katika utunzi wake wa nyimbo za injili. Sasa kwamba Kenya ni jirani ya Tanzania, kuna haja ya kujikakamua na kuangalia ni kwa njia gani ambayo tunaweza kukuza muziki wetu kwa kutumia Kiswahili sanifu katika utunzi wa nyimbo na kuwasilisha maudhui ya nyimbo zenyewe. Baada ya Kenya kuidhinisha katiba mpya na kuifanya lugha ya Kiswahili kuwa lugha rasmi mwaka wa 2010, tunaweza kujivunia kuwa Kenya inaweza kuwa katika mstari wa mbele kukuza Kiswahili. Makala hii itachunguza nyimbo kadhaa za mwimbaji huyu na kuonyesha jinsi zinavyowasilisha maudhui. Hiki kinaweza kuwa kielelezo kwa wasanii wengine wa muziki.

Mchango wa Tume za Elimu Nchini Kenya katika Kukuza Lugha ya Kiswahili

Gladys Kinara: glamoke@yahoo.com, Japheth Peter Muindu: pejamuindu@yahoo.com, Edwin Masinde: emasinde2000@yahoo.com, Jackline moraa: jacklinemoraa88@yahoo.com, Chuo Kikuu cha kenyatta

Nchi ya Kenya ina lugha zaidi ya arobaini. Kutokana na wingi huu wa lugha, kuna tamaduni tofauti. Kumekuwa na sera tofauti za lugha zinazolenga kutafuta lugha inayoweza kufanikisha mawasiliano nchini na kuleta umoja wa jamii hizi ili kufanikisha shughuli za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Bila lugha, mawasiliano hayawezi kuwepo na mtagusano pia hauwezi kuwepo. Lugha hufanikisha shughuli zote katika jamii. Iwapo jamii inataka kuendelea, kuna haja ya kufanikisha mawasiliano ili kukuza shughuli mbalimbali zinazoendelea. Kwa mfano, ili elimu ifaulu katika mazingira yenye wingi lugha, kuna haja ya kuwa na lugha ya kufundishia. Makala hii inalenga kuchunguza tume tofauti za elimu nchini Kenya ili kuweka bayana mchango wao katika kukuza lugha ya Kiswahili na hasa katika kuleta umoja. Sampuli ya kimaksudi itatumiwa. Data itachanganuliwa kulingana na malengo ya makala hii kwa kuzingatia mabadiliko ya jamii ambayo yanaonyesha haja ya kuwa na mapendekezo mapya kukidhi mahitaji ya jamii hasa ikizingatiwa kuwa jamii imeendelea katika nyanja tofauti kama vile utandawazi. Mabadiliko mengine ni kama vile maajilio ya katiba mpya. Kuna haja ya kuchunguza tume hizo na kupendekeza njia zinazoweza kutumiwa kupanua matumizi ya lugha ya Kiswahili.

Utata wa Uainishaji Virai katika Mtaala wa Shule za Upili Nchini Kenya

Gladys Kinara: glamoke@yahoo.com, Pius Nyakundi: nyakundipius@yahoo.com, Pamela M. Y. Ngugi: muhadiap@yahoo.com, Chuo Kikuu cha Kenyatta

Mojawapo wa mada mpya zilizojumuishwa katika silabasi ya sasa ya Kiswahili katika shule za upili nchini Kenya ni virai. Hapo awali, dhana ya virai ilifundishwa katika baadhi ya kozi za isimu kwenye vyuo vikuu. Ingawa hatua hii imechangia pakubwa katika ukuzaji wa viwango vya kisarufi miongoni mwa wanafunzi, upo utata unaojitokeza katika jinsi ilivyosawiriwa vitabuni. Fasili za dhana yenyewe katika vitabu vya kiada vivavyotumika sana zinatofautiana. Isitoshe, baadhi ya mifano inayotolewa kushadidia aina za virai inakinzana na vijejezi vinavyotangulia. Hali hii inawakanganya sio tu wanafunzi bali pia walimu wanaotarajiwa kuwaelekeza wanafunzi hawa. Makala hii inalenga kuchunguza maana ya virai, kuweka wazi mifano ya virai katika lugha ya Kiswahili na kupendekeza njia mwafaka zinazoweza kutumiwa na walimu pamoja na wanafunzi ili kuondoa utata huu na kufanikisha ufundishaji wa dhana hii katika lugha ya Kiswahili.

Tafsiri na Uenezaji wa Kiswahili: Mifano kutoka katika Tamthilia za Steven Kanumba

Hadija Jilala, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania: dijaah@yahoo.com au Hadija.jilala@out.ac.tz

Makala haya yanachunguza juu ya tafsiri na uenezaji wa Kiswahili kwa kutumika mifano ya tamthilia za Steven Kanumba. Tafsiri ni daraja na kiungo cha mawasiliano baina ya jamii za tamaduni tofauti. Tafsiri sadifu huweza kufanikisha mawasiliano kukuza na kueneza lugha na wakati huo tafsiri ambazo si sadifu huweza kuleta matatizo katika maana na ujumbe wa matini chanzi. Hivyo lengo la makala haya ni kuchunguza jinsi tafsiri inavyotumika katika kueneza lugha ya Kiswahili kwa kutumika tamthilia za Steven Kanumba. Malengo mahususi ya makala haya ni kubainisha dhima ya tafsiri katika katika tamthilia za Kiswahili, kubainisha changamoto za tafsiri ya Kiswahili kiingereza katika tamthilia za Kiswahili na kupendekeza mbinu za kuboresha tafsiri ya Kiswahili Kingereza katika tamthilia za Kiswahili. Nadharia ya skopos imetumika katika kuchunguza, kuchambua na kujadili data za makala haya.

Utamaduni Katika Tafsiri: Uchunguzi wa Mbinu za kutafsiri matini za Kiutamaduni za Kiswahili-Kiingereza

Hadija Jilala , Chuo Kikuu Huria cha Tanzania , Dar es Salaam, Tanzania: dijaah@yahoo.com au Hadija.jilala@out.ac.tz

Mbinu za tafsiri ni hatua zinazopelekea kwenye suluhisho la tatizo la tafsiri. Kwa mujibu wa Lorsch (1991:76) kama alivyonyukuliwa katika Chesterman (2005) mbinu za tafsiri ni mbinu zinazofahamika kama suluhisho la tatizo ambalo mtu anakumbana nalo anapotafsiri maneno yaliyopo katika matini kutoka katika lugha moja kwenda katika lugha nyingine. Makala haya yanajadili juu ya mbinu zinazotumika kutafsiri maneno ya kiutamaduni kutoka katika lugha ya Kiswahili kwenda katika lugha ya Kiingereza. Lengo kuu la makala haya ni kufanya uchunguzi wa kina juu ya mbinu zinazotumika kutafsiri maneno yaliyofungamana na utamaduni kutoka katika lugha ya Kiswahili kwenda katika lugha ya Kiingereza. Malengo mahususi ni; kubainisha mbinu zinazotumika kutafsiri maneno ya kiutamaduni, kuibua mbinu inayotumika zaidi kutafsiri maneno ya kiutamaduni katika matini za kitalii, kubainisha mbinu inayofaa kutafsiri matini za kiutamaduni kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza na kubaini sababu ambazo zinasababisha kutumia mbinu hiyo zaidi ya mbinu zingine katika kutafsiri maneno ya kiutamaduni katika matini za kitalii. Mbinu za kutafsiri matini za kiutamaduni zilizopendekezwa na Newmark (1988) na (2003) zilitumiwa kama mwongozo wa kubainisha mbinu zinazotumiwa kutafsiri maneno ya kiutamaduni kutoka katika lugha ya Kiswahili kwenda katika lugha ya Kiingereza.

Mstakabali wa Kiswahili na Maendeleo ya Jamii

Inyani Simala, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro

Makala haya yanasherehekea ufanisi wa Kiswahili nchini Kenya kwa kutazama mstakabali wake katika kuiendeleza nchi. Kwa kutambua umuhimu wa Kiswahili, makala yanahoji kuwa lugha hii ina dhima kuu ya kufanikisha kila aina ya hatua ifaayo kuhakikisha maendeleo endelevu.

Miaka Hamsini ya Maendeleo ya Kiswahili katika Elimu Nchini Kenya

Isaac Ipara Odeo, Chuo Kikuu Kishiriki cha Kibabii: iparaodeo@yahoo.com

Kenya ilipopata uhuru wa bendera mwaka wa 1963 mwandishi wa makala haya alikuwa mwanafunzi wa darasa la pili shule ya msingi. Tangu lugha hii ilipobainishwa kama lugha yenye dhima kielimu wakati huo, imekabiliwa na mikumbo mingi. Imetetewa na wapenzi wengi kuanzia rais wa kwanza wa Jamhuri ya Kenya, Mzee Jomo Kenyatta mbele ya wapinzani wake lukuki na wenye uwezo mkubwa. Hata hivyo, lugha hii imekwepa vikwazo vyote hadi kuondokea kuwa lugha ya kitaaluma katika vyuo vikuu. Naazimia katika makala haya kujadili, kuweka wazi na kukumbusha baadhi ya matukio katika kipindi cha nusu karne ya maendeleo ya Kiswahili.

Ufundishaji wa Kiswahili Ughaibuni: Maendeleo na Changamoto

Kiarie Njogu, Chuo Kikuu cha Yale, Marekani

Katika kuadhimisha maendeleo ya Kiswahili katika kipindi cha miaka 50 ya uhuru nchini Kenya, ni muhimu kuchanganua maendeleo hayo pia nje ya Kenya na eneo pana la Afrika ya Mashariki. Ufundishaji wa Kiswahili nje ya Afrika ya Mashariki umechochewa na mambo mabalimbali kama vile siasa na matukio tofauti ya kihistoria. Wakati wa kinyang'anyiro cha kugawana na kutawala Bara la Afrika kimabavu, Wajarumani walianzisha taasisi

za kufundisha Kiswahili kwa viongozi walioletwa Tanganyika. Taasisi hizi ziliendelea kutoa mafunzo ya Kiswahili hata baada ya Ujerumani kuipoteza Tanganyika baada ya Vita ya Kwanza ya Dunia. Katika mivutano ya Dola kuu kabla ya kuvunjika kwa Umoja wa Sovieti, lugha ya Kiswahili ilifundishwa kwa wageni kama njia moja ya kupenya na kuufahamu utamaduni wa wasemi wa lugha hii na kuzuia mataifa hayo machanga kuegemea upande Fulani wa siasa- wakati huo ushindani mkubwa ukiwa baina ya mlengo wa kibepari na ukomunisti. Katika karatasi hii, tutaangazia maendeleo ya ufundishaji wa Kiswahili nje ya Afrika ya Mashariki (na hasa Marekani) katika kipindi cha miaka 50 iliyopita. Changamoto ambazo ufundishaji wa lugha ya Kiswahili katika mataifa ya nje umekumbana nazo zitajadidiliwa na kuhitimisha kwa kutoa mapendekezo ya kukabiliana na changamoto hizo.

Mwanafunzi wa Kigeni na Mkanganyiko wa Kiistilahi na Kisemantiki katika Kiswahili cha Tanzania Bara na Zanzibar

Musa Mohamed Salim Shembilu, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu ch Dar es Salaam:
mumoshe2006@yahoo.com

Wanafunzi wa kigeni wamekuwa wakija Tanzania makundi kwa makundi na kutoka katika nchi mbalimbali zilizopo katika Bara la Afrika na nje ya bara hili. Wanafunzi hawa huja kwa lengo la kujifunza Kiswahili, katika ngazi ya awali au ngazi ya kati na juu. Huja wakiamini kuwa katika eneo la Afrika Mashariki ndiyo mazingira halisi ya kujifunza Kiswahili sanifu. Hata hivyo, katika eneo hili la Afrika Mashariki kumekuwapo na tofauti kubwa za kimsamiati na kisemantiki katika matumizi ya maneno hayo ya Kiswahili. Hutokea kwamba msamiati unaotumika mathalani Kenya kuwakilisha dhana X umekuwa tofauti na msamiati utumikao Tanzania kuwakilisha dhana hiyohiyo. Mfano eneo la uchaguzi kwa ajili ya kumpata mbunge, nchini Kenya huliita 'kaunti' ilhali katika Tanzania huliita 'jimbo'.

Tofauti hizi za kimsamiati na kisemantiki zimekuwa zikileta mkanganyiko mkubwa kwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama lugha yao ya pili. Lengo la makala haya ni kubainisha mkanganyiko unaowakumba wanafunzi wa kigeni wanaojifunza Kiswahili kutokana na tofauti zilizopo za kimsamiati na kisemantiki katika Tanzania bara na Zanzibar.

Makala haya yatamnufaisha mwanafunzi mgeni kuwa mwangalifu anapojifunza na kutumia Kiswahili katika mazingira ya Tanzania bara na Zanzibar.

Si hivyo tu, bali makala haya yatatia msukumo wa kushirikiana kwa wataalamu wa Kiswahili wa Afrika Mashariki, Afrika na Ulimwengu kwa ujumla katika kuondoa tofauti za kimsamiati na kisemantiki zilizozopo.

Kifanywe Nini Kiswahili ili Kifanye Nini?

Njoroge Ngugi

Kiswahili ndio lugha yenye wasemaji wengi mno kusini mwa sahara. Ni lugha ya kitaifa nchini Tanzania na Kenya pamoja na kuwa ina tumika mno Uganda, Rwanda, Burundi, Taifa la Congo na Comoros. Inaaminika kuwa na wasemaji wanaozidi watu milioni mia moja. Ndio lugha pekee ya kiasia inayohesabika kama mojawapo katika lugha rasmi za Umoja wa Afrika. Ughaibuni, Kiswahili kinafunzwa katika zaidi ya vyuo vikuu hamsini, si marekani, si uropa, Si bara Hindi.

Lugha yenye usemaji kama wa Kiswahili inafaa kuwa kiungo kati ya tamaduni anuai, iwe daraja inayowaunganisha wasemaji hawa badalia, ikawaruhusu kubadilishana amali za kitamaduni, mawazo, na ujuzi na kujenga jamii yenye ubadalia (polycentric society). Kiswahili ndio lugha inayofaa kutumika katika kutoa picha na ufahamu wa ulimwengu mzima kuhusu Afrika. Lakini hili linatokea? Linatendeka?

Makala hii inatalii nafasi hii iliyo nayo lugha ya Kiswahili pamoja na kuchanganua juhudi na upungufu wa washika dau wa lugha hii katika viwango vya kibinafsi, kitaasisi na hata kitaifa katika kukipa Kiswahili nafasi na mwanya wa kutekeleza majukumu haya.

Sheng na Kiswahili sanifu: Rasilimali au Kiangamizi

Peter Githinji, Chuo Kikuu cha Ohio, Marekani

Kwa mda mrefu, watetezi wa Kiswahili wamekuwa wakilalamika kwamba msimbo wa Sheng ni kikwazo kikubwa katika ukuzaji na uendelezaji wa Kiswahili, hasa katika maeneo ya mijini ambako msimbo huu umetia fora. Katika makala hii, ninadai kwamba kusambaa kwa Sheng hakukihatarishi Kiswahili, ila sera zetu na ufundishaji wetu wa Kiswahili ndio wenye kasoro. Pia nitajadili jinsi Sheng imechangia katika kuendeleza matumizi ya Kiswahili katika mikatadha ambayo ingetwaliwa na Kiingereza au lugha za kiasili. Nikirejelea historia ya chimbuko la msimbo huu iliyoanza wakati nchi yetu ilipokuwa ikijikomboa kutoka kwenye minyororo ya ukoloni, nitazungumzia kuhuzu jinsi Sheng ilitumia muundo wa Kiswahili katika ubunifu wake na hivyo kupanua matumizi ya Kiswahili mjini Nairobi wakati baadhi ya viongozi walikuwa wakipigia debe Kiingereza badala ya Kiswahili. Nachukua msimamo wa Chege Githiora kwamba Sheng ni mojawapo ya lahaja chipukizi za Kiswahili na kama vile lahaja kongwe za Kiswahili hurutubisha Kiswahili badala ya kukiua, Sheng inaweza kukirutibisha Kiswahili hasa katika ulimwengu wa teknohama na utandawazi. Badala ya kuiona Sheng kama zimwi lililokuja kukiangamiza Kiswahili, ninawahimiza waalimu wa, na wadau wa Kiswahili wabadilishe mtazamo wao na waelekeze juhudi zao katika kuunda mbinu nzuri za ufundishaji wa Kiswahili sanifu. Nitahitimisha kwa kusema badala ya kuipiga vita tunahitaji kuielewa lahaja hii mpya zaidi.

Makundi ya Lugha na Fasihi kwenye Facebook

Rachel W. Maina, Chuo Kikuu cha Mount Kenya

Lugha ya Kiswahili imetamba katika nyanja za teknolojia ya habari na mawasiliano. Kitandazi cha facebook hutumiwa na mamilioni ya watu kuwasiliana. Wahusika huwa na akaunti za kibinafsi au akaunti za makundi. Mojawapo ya maeneo ambapo Kiswahili kinatumika sana kwenye facebook ni katika makundi ya mijadala kuhusu lugha na fasihi ya Kiswahili. Baadhi ya makundi haya yameibuka kutokana na vipindi maarufu redioni nchini Kenya, mathalani Bahari ya Lugha (Radio Citizen) na Nuru ya Lugha Radio Maisha (Radio Maisha). Washiriki huuliza maswali ambayo hujibiwa kwenye vipindi hivi. Mengine hujibiwa na wanachama wa makundi hawa kwa mtindo wa mdahalo. Makundi mengine ni juhudi za watu binafsi, kama vile Umbuji na Ulimbwende wa Lugha ya Kiswahili, Michapo Uswahilini, Msasa wa Lugha na Fani Husika, Jamvi la Fasihi na mengineyo. Utafiti huu utangazia mada mbalimbali zinazojadiliwa katika makundi ya Bahari ya Lugha, Umbuji na Ulimbwende wa Lugha ya Kiswahili na Nuru ya Lugha Radio Maisha. Makundi haya yana washiriki wengi na kila siku maswali mengi hujadiliwa mle. Aidha, mtafiti atalenga kuonyesha sifa za washiriki kama vile kiwango cha elimu, jinsia na umri. Utafiti huu utachangia dafina ya tafiti kuhusu matumizi ya Kiswahili katika TEHAMA na pia maoni kuhusu lugha hii kwa jumla.

Nafasi ya Kiswahili katika Utekelezaji wa Rajua 2030: Tathmini ya Kipindi cha Awali 2008 – 2012

Sheila Ali Ryanga, Chuo Kikuu cha Methodist, Bewa La Mombasa

Kama lugha ya taifa Kiswahili kinahitajika kutekeleza mengi miongoni mwa watumizi wake nchini. Lugha hii inatumika sokoni, majumbani inakuwa lugha ya kwanza ya watoto mijini, imekuwa lugha badalia inayokubalika katika jopo la lugha baada ya mtihani wa kidato cha nne, kwa uteuzi wa masomo vya uoni ama kuomba ajira; somo la lazima katika madaraja yote ya shule; lazima kufanya mtihani wa Kiswahili kwa wagombea ubunge. Kwamba ni lugha inayowahusisha watu wa makabila tofauti na kuendeleza biashara mipakani mwa mataifa mbalimbali ni uhalisia usiokanushika. Biashara kama hizi hutegemea rasimili za nchi husika, ustawi wa viwanda, ustawi na amani katika kanda, miundo mbinu ya usafiri na ujuzi na maarifa kwa wataalamu. Ingawaje, ikiwa raia wa nchi waliowengi hawajafahamu mengi yanayoendelea ama yaliyopangwa katika Mpango Mkakati wa nchi, ulio na lengo kuu la kufifisha umaskini miongoni mwa raia, basi mazuri yote yanayopendekezwa katika Rajua 2030 hayataweza kufikiwa, ama yanapofikiwa kwa kiwango Fulani, hayatanufaisha wengi. Hili linapotukia, huendeleza umwinyi, ukabaila and ubwenyene, unaokandamiza kwa chuki zaidi kupita ukoloni. Zaidi hufifisha lugha na kukejeli katiba ya nchi. Makala hii itachunguza nafasi iliyochukuliwa na lugha hii katika kipindi cha kwanza cha Ruwaza 2030 nchini Kenya kufanikisha lengo kuu la ruwaza hiyo katika kupunguza umaskini na kuwawezesha raia kiuchumi.

Lugha Tamathali katika Habari za Soka: Mifano ya Matumizi katika Magazeti ya Kiswahili

Kevogo Stanley Adika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Stella Maris Mtwara, Chuo Kishiriki cha Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino, Mtwara, Tanzania: surayangu@gmail.com

Soka ni mojawapo ya michezo maarufu mno ulimwenguni. Umaarufu huu unaweza kuhusishwa na historia yake ndefu pamoja na wepesi wa kutambua mshindi na mshindwa miongoni mwa mashabiki wa matabaka mbalimbali. Hata hivyo, mashabiki wa soka hutegemea usasa, usahihi na usisimujaji wa ripoti na changanuzi za mechi za viwango na daraja anuwai. Kwa kipindi kisichopungua miongo mitano, lugha ya Kiswahili imepata umaarufu kama lingua franca muhimu ya kupashana habari anuwai zikiwemo za spoti. Inatumika kwingi katika vyombo vya mawasiliano ya umma kama vile redio, runinga, magazeti, majarida, intaneti. Isitoshe, mawasiliano yanayohusisha tarakilishi kama vile mitandao ya kijamii, blogu, soga na milisho ya RSS pia inatumia Kiswahili katika kuwasilisha taarifa mbalimbali. Pamoja na kuikuza kimsamiati, kiistilahi na kisajili, mawasiliano ya aina hii pia ni chachu ya kuikuza lugha ya Kiswahili kihadhi na kutanua wigo wake kimatumizi. Kwa kutumia data iliyodondolewa kutokana na kongoo ya magazeti manne ya Kiswahili – Dimba, Championi, Mwaspoti na Taifa Leo, makala hii inanua kuchuguza matumizi ya lugha tamathali katika ripoti na changanuzi za soka. Tunachambua namna ambavyo wanahabari hutumia lugha kitamathali kueleza matukio matatu muhimu kwenye mchezo wa kambumbu, yaani kushinda, kushindwa na kutoka sare. Tunahoji ni taswira zipi zinazojitokeza? Lugha tamathali inatumikaje kama mbinu ya kupasha habari za soka kwa usahihi na kumvutia msomaji.

Miaka Hamsini ya Fasihi ya Kiswahili Nchini Kenya: Maendeleo, Changamoto na Mustakabali Wake

Alex Umbima Kevogo, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino cha Tanzania, Chuo Kishiriki cha Stella Maris Mtwara, Mtwara, Tanzania: alekevogo@yahoo.com, umbima2000@gmail.com

Mataifa mengi ya Afrika Mashariki Kenya ikiwemo, yanaposherehekea miaka hamsini ya uhuru, makala hii imechunguza historia na maendeleo ya fasihi andishi ya Kiswahili ya Kenya ndani ya kipindi cha miongo mitano baada ya uhuru. Hata hivyo, ili kuiweka historia ya fasihi andishi ya Kenya katika picha halisi ya historia ya

fasihi andishi kamili ya Kiswahili kwa jumla, makala itaieleza kwa kuilinganisha na hali iliyoko kwingineko katika mataifa ya Afrika Mashariki hususan nchini Tanzania na Uganda. Msisitizo maalumu umekitwa kwenye mikondo ifuatayo inayojitokeza: (a) Kuzuka kwa fasihi ya kizalendo ya kupigania uhuru (b) Kuibuka kwa fasihi inayoihakiki jamii (c) Chimbuko la fasihi pendwa na fasihi ya vijana (d) Kuibuka kwa fasihi ya kimajaribio (e) Athari za utandawazi na tafsiri za kazi za fasihi zenye asili ya kigeni. Haya yote yamezingatia mkabala wa kihistoria unaotathmini maendeleo ya kijamii, kisiasa, kitamaduni na kiuchumi nchini Kenya miaka hamsini baada ya uhuru.

Usawiri wa Mwanamke katika Hadithi Fupi za Kiswahili: Mfano wa Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine ya S.A. Mohamed

Elizabeth K. Mue na E.W. Masinde, Chuo Kikuu cha Kenyatta, elizabethkasau@gmail.com

Kwa muda mrefu sasa, ulimwengu umeshuhudia malalamishi kwamba mkabala wa kuumeni umetawala jamii nyingi za kilimwengu, jambo ambalo limesababisha kupuuzwa kwa wanawake. Kanuni nyingi za kidini, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni zimetumiwa katika kushadidia uwezo wa mwanamume na kumdunisha mwanamke. Kwa hivyo, suala la mwanamke ni mojawapo ya maudhui mengi yanayopatikana katika fasihi ya kiswahili. Wahakiki wanazidi kuangalia jinsi ambavyo mwanamke anasawiriwa katika fasihi na nafasi anayopewa katika maisha kwa jumla. Kama asemavyo Wandera (2002:80), maswala ya kijinsia ni ya kimsingi katika maisha ya mwanadamu. Kwa mujibu wa Mdee na Mwansonko (2000), kupuuzwa kwa hadithi fupi kunajitokeza zaidi katika uwanja wa uhakiki. Kwa hivyo, ni maoni yetu kwamba wahakiki wengi wa fasihi ya kiswahili hawajashughulikia utanzu huu wa hadithi fupi kwa kina. Makala hii inanua kuchunguza na kujadili jinsi ambavyo mwanamke amesawiriwa katika Arusi ya Buldoza na Hadithi nyingine. Itaonyesha iwapo hadithi fupi za kiswahili zimetumiwa ili kuunda upya uhalisi wa mwanamke kwa kupangua na kudhihirisha miundo ya kijadi ambayo inamtukuza mwanamume na kumkandamiza mwanamke.

Utandawazi na Ufundishaji wa Kiswahili kwenye Ulimwengu

Mbwarali Kame, Chuo Kikuu cha Moi: dktabuyaasir@gmail.com

Tunapo angalia ulimwengu wa sasa twapata yakuwa kuna mengi ambayo yameibuka na hasa kwenye suala la mawasiliano na Utandawazi, ni hivi majuzi tu ambapo suala la utandawazi lilijadiliwa kwa kina kwenye makongamano tafauti na ikawa suala la lugha ni kigezo kikubwa cha kujadiliwa kwenye makongamano kama hayo. Kwa hakika lugha ndio kioo muhimu kwenye ulimwengu wa utandawazi ni lugha nyingi zimewekwa kwenye kila chombo kinacho shughulikia utandawazi kwenye ulimwengu kama huu. Kiswahili ni lugha pana sio kwa nchi za Africa Mashariki bali kwa ulimwengu mzima ni lugha iliyo tambulika na wengi na hata kuingizwa lugha ya Kiswahili kwenye tarakilishi mbali mbali na kwenye mitandao. Katika makala haya tutajadili suala la utandawazi na kuchunguza dhana ya utandawazi wenyewe kwenye dunia hii ya sasa, pamoja na kuchunguza kwa kina namna ya lugha ya Kiswahili ilivyo tumika na sasa inavyo tumika kwenye suala la utandawazi, pia namna utandawazi ulivyo ikuza lugha ya Kiswahili na maendeleo yanayo tarajiwa kwa lugha ya Kiswahili kwa kuibuka mifumo ya utandawazi kwenye ulimwengu kama huu. Pia tutaangazia lugha ya Kiswahili namanuafaa katika taaluma, na jamii na uchumi kwa utangulizi huu nafikiri itakuwa nimefikia malengo ya kongamano la CHAKITA.

Je, Sheng ni Lahaja ya Kiswahili?

Ayub Mukhwana, Chuo Kikuu cha Nairobi

Kuwepo kwa lughapendwa ya Sheng Kenya si suala linalohitaji mjadala. Kwa kuwa lugha hii ipo, utafiti kuhusu pia ni halali. Utafiti kuhusu lugha hii kwetu unatokana na hali ya kutokuwepo kwa maafikiano kuhusu hasa chanzo na unasaba wa lugha hii. Nadhariatete zilizotolewa kuhusu suala hili zinaiona lugha ya Sheng kama lugha kipindi ya Kiswahili, kama lahaja ya kijamii ya Kiswahili, au kama kinyemeleo tu cha kilugha ambacho hakina msingi. Hizi nadhariatete zimetolewa kihisia kwa kukosa kujikita katika nadharia yoyote maalumu. Kwa hiyo tunadhamiria kutoa kauli yetu kuhusu chanzo na unasaba wa Sheng kwa kujikita katika nadharia za ujifunzaji na utumizi wa lugha za Kisosholojia na Kisoshosaikolojia.

Miziki ya Kiswahili kama chombo cha Kuhimiza Suala la Uwajibikaji katika Jamii: Nyimbo za Baraka Mwinshehe

Henry Indindi, Chuo kikuu cha Nairobi

Katika miaka hamsini ya uwepo wa taifa la Kenya na kuthaminika kwa Kiswahili kama lugha yake ya taifa, na sasa tena ya kwanza rasmi, ni muhimu kutambua kwamba kuna mambo mengi muhimu ambayo Kiswahili na walezi wake wamejaribu kushughulikia. Waandishi wa fasihi ya Kiswahili, watunzi na waimbaji wa miziki ya Kiswahili wametumia vyombo hivyo vya sanaa kuadilisha na kupendekeza hulka ambazo raia wenzao wanapaswa kuwa nazo katika kuimarisha uwepo na maendeleo ya kiuchumi ya jamii hizi. Kizazi cha sasa na inavyoelekea kijacho, ni vizazi ambavyo vimekumbwa na matatizo mengi ya kutowajibika kutokana na mambo mbalimbali.

Kwanza, hamu ya kuishi ughaibuni kwa kuepuka kazi zinazodaiwa kuwa chafu na ujira unaominika kuwa usiotosha ni moja katika ndaro zinazovikabili vizazi vya sasa. Vijana wengi hutamani kutorokea ng'ambo ili kuepuka 'umaskini' wa kwao. Aidha, kizazi cha sasa kimeteleza kabisa kwa kujihusisha na ulevi na utumizi wa dawa za kulevya katika nyakati na mazingira yasiyofaa. Matokeo yake yamekuwa kutelekeza familia zao na kuvunjika kwa ndoa nyingi hata katika miezi michache tu baada ya kuoana.

Hali hii kwa kweli inasikitisha na kwa wazazi na serikali kwa jumla inayolazimika kuingilia kati na kulainisha mambo ili kuepuka mizigo ya baadaye wanalazimika kujikuna vichwa ili kupata mbinu zitakazowasaidia kuzuia hatari kabla ya kutukia. Cha kusikitisha ni kwamba ingawa wengi tunapenda burudani na miziki, wengi hufurahia midundo lakini hatuchunguzi ujumbe unaopatikana katika tungo hizo. Maudhui katika utungo wowote ndicho kigezo cha kimsingi kupima kama mtunzi amefaulu au hakufaulu. Nyimbo za Baraka Mwaruka Mwinshehe kwa jumla zina maudhui mazuri sana. Haya ni pamoja na maudhui ya Uwajibikaji ambayo yanaelekea kupuuzwa na vizazi vya sasa.

Karatasi hii hivyo basi inanua kuonesha jinsi mtunzi na mwimbaji huyu aali mwendazake alivyoihimiza jamii kuwajibika kwa kutumia nyimbo zake. Nitatumia nyimbo mbili za Mwinshehe kudhihirisha jinsi alivyoshughulikia uwajibikaji katika uzalendo, starehe na ndoa.

Ufundishaji wa Kiswahili katika Nchi za Kigeni: Mfano wa Chuo Kikuu cha Syracuse

Miriam Osore na Brenda Midika, Chuo Kikuu cha Kenyatta: kenyanimo@yahoo.com, midikabrenda@gmail.com

Ufundishaji na ujifunzaji wa lugha za Kiafrika katika nchi za kigeni una historia ndefu. Kwa mujibu wa Moshi katika (Eyamba G. et al, 2011: 26-27), ufundishaji wa lugha za Kiafrika haukuanzia madarasani bali ulianzia nyanjani katika karne ya 15 ambapo wamishenari walitaka kujua zaidi kuhusu lugha za jamii walizokuwa

wakieneza injili. Walianza kwa kuandika makamusi na vitabu vya sarufi ambavyo viliwahamasisha wanaisimu kama vile Wilhelm Bleek ambaye alichapisha kitabu A Comparative Grammar of African Languages. Miongoni mwa wanaisimu wengine ni kama James Frederick Schon (1862) na Carl Meinhoff (1899) ambaye alichapisha kitabu cha fonolojia ya lugha za Kibantu na Johann Ludwig Krapf (1850) aliyechapisha kitabu cha kwanza cha sarufi ya Kiswahili. Mafunzo ya lugha za Kiafrika kule nchini Marekani yalianzishwa miaka ya 1950, kama kipengele muhimu cha sheria ya Taifa The National Defense Act ya 1958 ambayo ilianzisha vituo vya mafunzo ya Afrika (Dougherty, 1993). Mafunzo haya yalikusisha hasa lugha na fasihi. Kuanzia wakati huo vyuo nchini Marekani vimekuwa vikifunza lugha za Kiafrika ikiwemo lugha ya Kiswahili. Makala haya yanalenga kufafanua ufundishaji wa lugha ya Kiswahili nchini Marekani, mfano wa Chuo Kikuu cha Syracuse. Yatagusia mbinu za ufundishaji kwa mfano, matumizi ya teknolojia na changamoto walimu wa Afrika wanakumbana nazo katika kufundisha Kiswahili kwa wazungu. Mwisho yatapendekeza jinsi ya kuboresha ufundishaji wa Kiswahili kwa wasomaji wasio katika mazingira halisi ya matumizi ya lugha hiyo.

Miaka Hamsini ya “Leso” Mjini Mombasa : Kitambulisho cha Mswahili

Mwanakombo Mohamed, Chuo Kikuu cha Moi

Kitamaduni nguo anazovaa mtu husawiri nafsi na utu wake. Nguo zako hutujavya aila yako, hulka, jinsia na vile unavyotaka ulimwengu ukufahamu. Vazi lolote unalolivaa huzua maana kuambatana na muktadha ulioko. Kwa mwanamke Mswahili vazi la lesu au jinsi anavyojitanda lesu yake, huibua hisia nyeti miongoni mwa jamii. Hisia hizi hulilingana na muktadha maalum unaovaliwa lesu ile, aina ya lesu na maana ya fumbo lililoandikwa lesoni.

Katika makala hii, tunanua kuiangazia lesu kama vazi la Mswahili, kwa kutathmini utata wake, aina zake na hisia anazoibua anayezivaa. Zaidi, utafiti huu utachunguza iwapo lesu husawiri kitambulisho cha mwanamke Mswahili katika maisha yake. Vazi hili lilianzaje, limebadilika vipi, maendeleo yake ni yepi, na mustakabali wake ni upi?

Utafiti huu umechambua jinsi lesu zilivyochangia mitindo ya nguo za kiafrika na kupendekeza kuwa welewa huu ni thibitisho tosha la miaka hamsini ya kukua kwa utamaduni wa Mswahili.

Usiasa wa Lugha kama Mkakati wa Uchuuzi wa Sera za Kisiasa Katika Mdahalo wa Uraisii Februari 2013 Nchini Kenya

Florence Ngesa Indede, Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika Chuo Kikuu cha Maseno

Siasa za uchaguzi na hasa uchaguzi wa uraisii nchini Kenya mwaka wa 2013 zilivutia sana umakinifu wa kitaifa na kimataifa na hasa wakati wa mdahalo wa maraisii uliotendeka mwezi wa Februari mwaka 2013. Maandalizi na utekelezi wa mdahalo huu ni ishara mojawapo iliyoonyesha ukomavu na demokrasia ya kisiasa nchini Kenya ikichukuliwa kwamba hii ilikuwa ni mara ya kwanza tukio hili la kihistoria kutokea nchini. Ukomavu huu haungekamilika pasi na kuendeleza mdahalo huu katika Kiswahili jambo ambalo lilitazamiwa sana na Wakenya wazalendo. Lugha katika siasa ni mojawapo ya nyenzo maalum ambayo hutumiwa na wanasiasa na wafuasi wao katika ama kushawisi uungwaji mkono au kuua kabisa matumaini ya vyama pinzani katika kueneza na kusambaza sera zao. Ingawa siasa ndilo jambo ambalo katika sura ya nje lingeonekana wazi katika mdahalo huu, ni dhahiri kuwa lugha ilitumiwa kwa kiwango kikubwa kufinyanga hisi, fikra na mielekeo ya sera za vyama husika. Mchezo wa maneno ulitumiwa kama silaha kali ambayo kwa mapanana marefu iliuvutia upande mmoja au kutawanyisha kabisa ushirikiano wa kisiasa uliopo. Malumbano, uteuzi makini na maksudi ya lugha ni mbinu mojawapo ambayo ilitumika katika uchuuzi wa sera za ama Jubilee, CORD, Narc Kenya, Amani n.k katika

mdahalo wa uraisi. Wagombea uraisi wananane Uhuru Kenyatta, Raila Odinga, Musalia Mudavadi, Martha Karua, Peter Kenneth, Ole Kiyiapi, Paul Muite na Abduba Dida, walijitokeza kama viongozi shupavu wa vyama mbalimbali wakati walipojikakamua kujadili maswala pevu ya mifumo, sera, mielekeo na mipango yao ya baadaye wanalichaguliwa kuongoza Kenya. Tofauti na mikutano ya kisiasa, mdahalo ulitumiwa kama uwanja sawazishi uliowakutanisha watazamaji wa kitaifa na kimataifa katika kukagua semi, umilisi wa lugha na ukakamavu wa viongozi hawa katika kuchuuza sera zao. Mjadala huu ulitumiwa kama mthani mkubwa sana wa kudhihirisha umilisi wa maswala ya kisiasa na kijamii lakini katika lugha ‘ngeni’ ya Kiswahili. Udadisi wa wawaniaji kuhusu ujuzi wao wa maswala ya kiuchumi na kijamii, matukio ya kihistoria nchini na mbinu zinazotumiwa katika kutatua mizozo ya kisiasa ilibainika. Ili kushawishi, kunyakua ushindi na kuonyeshesha ubingua na ubabe katika sisiasa, mdahalo huu ulitumiwa kama uwanja sawazishi wa kuchanganua maswala maalum ya kiuchaguzi, ubainishaji wa ubingwa na ustadi wa mawasiliano, hasa kwa kuwawezesha watazamaji na wasikilizaji kujiamulia. Ingawaje muktadha wa mdahalo ni rasmi na unaothibiti uumbuaji wa taswira za wanasiasa mahasimu, kwa kiwango fulani matumizi ya uongo, lawama, ufinyanzi wa fikira na kutoheshimiana ni matukio yaliyodhihirishwa katika mdahalo huu. Mielekeo hii ilionekana kutumiwa kama mbinu maalumu ya uchuuzi na ubainishaji wa sera mbalimbali za vyama husika. Pasi na kwamba maneno mateule yalitumiwa kuelezea na kufafanua mielekeo na mipangilio ya kisera ya vyama hivi, malumbano yalionekana kama nyenzo na mbinu ya kuaibisha na kadarnasi ya umma jambo ambalo lilionekana kuathiri nafsi, uwezo na uthabiti wa wanasiasa husika. Hisia za kutoridhika, hamasa na maonevu ni mojawapo ya maonyesho na vitendo vilivyoonekana kutokana na athari za utumizi lugha. Wasilisho hili kwa hivyo linachanganua namna ambavyo wanasiasa hawa walivyolumbana katika mdahalo huu kwa kujadili taswira za umbuji na uumbuaji wa kisiasa kimazungumzo kupitia makombora mbalimbali yaliyorushwa baina ya wanasiasa hawa. Ni lengo la wasilisho hili kubainisha ubunifu wa kimawasiliano wa wanasiasa hawa katika kuwasilisha sera za vyama husika, uthabiti na uthibiti wa lugha ya kisiasa katika kuimarisha mamlaka ya kisiasa.

Miaka Hamsini ya Taswira ya Mwanamke katika Ushairi wa Kiswahili Nchini Kenya

Clara Momanyi, Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki

Baada ya Kenya kujipatia uhuru mnamo mwaka wa 1963, kumekuwa na maendeleo makubwa ya uandishi wa mashairi yanayosawiri hali na miktadha mbalimbali. Taswira ya mwanamke katika tungo hizi imeendelea kubadilika kutegemea mabadiliko ya kiitikadi yanayochochewa na hali halisi za kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na hata kisiasa. Matilaba ya makala haya ni kujadili na kutathmini mitazamo na rai za baadhi ya washairi ili kubainisha mchango wao ama katika utetezi au udunishaji wa mwanamke nchini Kenya tangu uhuru. Kutokana na upana wa mada yenyewe, wasilisho limejikita katika uchunguzi wa baadhi tu ya tungo zinazomsawiri mwanamke. Hivyo, ni washairi wachache ambao kazi zao zimehakikiwa ili kubaini vichocheo ambavyo huenda vinachangia katika mabadiliko tuyapatayo katika tungo za wasanii hao kiwakati. Waaidha, makala yameangazia kwa ufupi mustakabali wa utanzu huu katika dahari hizi, hususan mchango wake katika maendeleo ya mwanamke.

Utekelezaji wa Katiba: Mapendekezo ya Sera ya Lugha za Kenya

Kimani Njogu, Twaweza Communications

Ili kuendeleza na kuimarisha ufundishaji na matumizi ya Kiswahili nchini Kenya, pana haja ya kuunda sera ya lugha za Kenya na mikakati ya utekelezaji wake. Sera hiyo ni muhimu ili kutoa mwongozo wa hadhi, upangaji na ujifundishaji wa Kiswahili; lugha ambayo tangu 2010 imetambuliwa kama lugha ya taifa na lugha rasmi ya Jamhuri ya Kenya. Katika kikao hiki, tutajadili Rasimu ya Sera ya Lugha za Kenya na nafasi ya Kiswahili katika Sera hiyo. Pia tutachunguza baadhi ya asasi zitakazoundwa kupitia sera hii na majukumu yake.

Mikondo katika Utafiti wa Isimu Nafsia

Mosol Kandagor, Chuo Kikuu cha Moi na Salim-Sawe, Chuo Kikuu cha Kabianga

Makala hii inajadili maendeleo katika isimu-nafsia kama tawi la isimu. Sehemu mbili za ubongo zinajadiliwa hasa kwa kujikita katika ujifunzaji-lugha, uchakataji-lugha na matumizi ya lugha. Masuala anuwai ya kinyurolojia yanayohusiana na uchunguzi wa lugha na akili yanabainishwa ambapo mchango wao kwa ufafanuzi wa vipengee vya isimu nafsia unadhihirishwa. Viwango vya ukuaji wa binadamu hususan katika ubongo vinajadiliwa kwa mujibu wa upataji/ujifunzaji lugha huku vikifungamanishwa na mikondo ya tafiti za kiisimu. Maswali yanayohusu utendakazi wa akili za wanawingi-lugha yanajadiliwa kwa kulinganishwa na akili za wanaumojalugha. Hatimaye, makala imedhihirisha umuhimu wa uchunguzi wa isimu-nyurolojia kwa mujibu wa maendeleo ya isimu kokotozi. Aidha makala inadokeza haja ya kufanywa kwa utafiti ili kuyajibu maswali ya iisimu-nyurolojia yanayohitaji utafiti zaidi.

Kiswahili na maendeleo ya kiutamaduni: Utamaduni-hamishwa unavyodhihirika katika msamiati wa Kiswahili

P. I. Iribe Mwangi, Chuo Kikuu cha Nairobi, iribeh@gmail.com , iribe@uonbi.ac.ke

Chombo ambacho ‘husafirisha’ utamaduni ni lugha. Lugha ni sehemu muhimu katika mawasiliano yoyote yale ya binadamu kwa kuwa ni lugha itumiwayo kupitisha habari kutoka kwa kundi moja hadi lingine. Kupitia kwa mazungumzo na maandishi, hali ya maisha ya jamii fulani hupata njia wazi ya kuingia ama kwa kizazi kipya aukwa jamii tofauti. Mambo yanayopitishwa kwa kizazi kipya au jamii hiyo tofauti ni pamoja naimani za jamii fulani, tabia zake, ala zake pamoja na mambo mengine yanayomilikiwa na kikundi au jamii fulani. Mambo haya ndiyo yanayojumuisha utamaduni wa jamii husika na baadhi huwa halisia ilhali mengine huwa dhahania. Kupitia utamaduni, watu na makundi huwezakujitambulisha, kufuata taratibu za jamii na pia kutoa mchango wao kwa jamii hiyo. Vipengee vyote hivi hupitishwa kupitia lugha. Makala haya yataeleza kwamba kwa kuchunguza msamiati ulioingia katika lugha ya Kiswahili kutokana na ukopaji na utohozi, kuna uwezekano wa kuonyesha vipengee fulani vya utamaduni wa kigeni ambavyo tayari vimeigwa na wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili na pia kuonyesha kuwa vipengee hivyo kwa sasa vimekuwa sehemu ya maisha ya kila siku ya watumizi wa lugha ya Kiswahili. Vipengee hivyo vinadhihirisha kwamba kukopwa kwa tamaduni ni hali ambayo inaendelea ulimwenguni kote ambapo jamii zote huchangiana kiutamaduni. Kutokana na msamiati kopwa, inawezekana basi kusema kwamba kumekuwa na hali ya kuhamisha tamaduni za kigeni na kuzishirikisha katika ulimwengu wa watumizi wa Kiswahili. Ili kufafanua hali hii, makala haya kutachanganua msamiati kopwa kutoka nyanja tofautitofauti za utamaduni halisia na dhahania na msingi wake wa kinadharia umo katikamwelekeo wa mtagusano wa lugha.

Maendeleo na Dosari katika Upanuzi wa Msamiati wa Kiswahili

Rocha M. Chimerah, Chuo Kikuu cha Pwani

Wakati Kiswahili kiliposanifishwa mwanzoni mwa muongo wa 30 wa karne iliyopita (yaani karne ya 20), lugha hii ilionekana kuwa na maneno machache sana. Hii ilisababishwa na kuwa ni lahaja yake moja tu (lahaja ya Kiunguja cha mjini, iliyokuwa ikisemwa na watu wa nasaba bora, ambao wengi walikuwa Waarabu au watu wenye asili ya Kiarabu).

Kuitegemea lahaja hii peke yake katika kuisanifisha lugha nzima ya Kiswahili (jumba na Kimvita kichache sana) kulifanya lugha sanifu iwe na upungufu mkubwa sana. Jambo la kwanza kuliifanya lugha hiyo iwe na maneno mengi ya Kiarabu yaliyokuwa si ya lazima kuwemo ndani ya lugha nzima kwa vile menziwe ya kibantu yalikuwepo,

lakini haya yalipuuzwa. Sababu ya pili ni kuwa takriban watu wote waliohusika katika zoezi la kuisanifisha lugha walikuwa wazungu, tena wamishenari. Hawa walikataa maneno ambayo waliamua ya kuwa yataleta utovu wa adabu katika matamshi, kwa hivyo wakastahabu kutumia maneno ya Kiarabu au ya Kizungu badala yake, hasa ya Kitalini au Kiingereza. Tatu hawakufikiria kubuni maneno ambayo yangetumika katika nyanja ngeni, kama vile teknolojia, kwa sababu lengo lao kuu lilikuwa kukitumia Kiswahili sanifu kueneza injili na kufundishia.

Sasa wanaisimu wa Kiafrika wamelazimika kubuni maneno katika nyanja zilizokosa kushughulikiwa zama hizo. Kwa jumla wamefanya kazi nzuri. Hata hivyo, kwa sababu wametakikana kufanya kazi kubwa, tena kwa msukumo mkubwa ajabu, kumetokea dosari nyingi katika uundaji wa maneno mapya, hasa kwa vile aghalabu hawajafuata mbinu za kiisimu zijulikanazo katika kubunia maneno ya lugha. Wakati umewadia wa kuzipiga msasa mbinu za kubunia maneno ilimradi kuhakikisha ya kwamba msamiati upatikanao ni wenya kueleweka kwa wepesi na wenye kuisema lugha hii, hususan wale ambao hii ndiyo lugha yao asilia (ulimi wa mama).

